GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXII Nam. ..... **29 Agosti, 2016** **Bei Shs. 5,000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti *Hutolewa kila Ijumaa*

YALIYOMO *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali Nam. 9 ya Mwaka 2005 na kutungwa Sheria inayoanzisha Mamlaka ya Manunuzi na Uuzaji Mali za Umma na kuweka Masharti mengine yanayohusiana na hayo..... 000

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili

Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali Nam. 9 ya Mwaka 2005, na kutunga Sheria mpya.

T A N G A Z O

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 21 Septemba, 2016 kwa kusomwa kwa mara ya kwanza na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

ZANZIBAR
29 Agosti, 2016

(Dkt. ABDULHAMID Y. MZEE)
Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

MSWADA

wa

SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MANUNUZI NA UUZAJI WA MALI ZA SERIKALI NAM. 9 YA MWAKA 2005 NA KUTUNGWA SHERIA INAYOANZISHA MAMLAKA YA MANUNUZI NA UUZAJI MALI ZA UMMA NA KUWEKA MASHARTI MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Umma ya 2016, na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri ataitangaza kwa kutoa taarifa katika Gazeti Rasmi la Seriklai.

Matumizi ya Sheria.

2.-(1) Sheria hii isipokuwa kama itaelezwa vyenginevvyo, itatumika kwa-

(a) manunuzi yote na uuzaji wa mali za Serikali yatakayofanywa na taasisi za inayofanya manunuzi na uuzaji mali za Serikali;

(b) fedha zote za umma-

(i) zinazotoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina na fedha maalum zinazotumika kupitia bajeti ya kazi za miradi au matumizi ya kawaida;

(ii) ambazo zimeainishwa kutumika kwa malengo na madhumuni ya nje, isipokuwa fedha zote ambazo zinaweza kutumika kwa malipo ya uwanachama au michango; na

(iii) za taasisi ya manunuzi na uuzali mali za Seikali;

(c) fedha zinazotumiwa katika mfumo wa mashirikiano na taasisi nyengine au zinazofadhiliwa au fedha zozote ambazo zina matumizi sawa ndani ya makubaliano ya mpango wa washirika wa maendeleo katika kutekeleza miradi ya kitaifa;

(d) manunuzi na uuzaji kwa taasisi inaoyofanya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali ndani au nje ya Zanzibar;

(e) manunuzi yanayofanywa kwa kutumia fedha maalum zilizotajwa katika aya ya (b), kwa taasisi ambayo siyo ya Serikali;

(f) manunuzi na uuzaji wa mali kwa kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni, ambapo taasisi ya umma ina hisa nyingi katika kampuni hiyo.

(2) Kwa madhumuini ya kuondoa shaka, kazi zifuatazo kwa taasisi za manunuzi na uuzaji wa mali za Serikali zitakuwa sio manunuzi ambayo yatafanywa kwa kutumia Sheria hii-

(a) upatikanaji wa mali au mitambo, pale ambapo mali au mitambo hiyo imeondoshwa na taasisi nyengine ya manunuzi na uuzaji wa mali za Serikali kwa kutumia Sheria hii;

(b) upatikanaji wa huduma kwa taasisi nyengine ya manunuzi na uuzaji wa mali za Serikali, isipokuwa kwa zile huduma zilizotolewa bila ya malipo na taasisi nyengine ya manunuzi na uuzaji wa mali za Serikali; na

(c) upatikanaji wa huduma hiyo umefanywa na muajiriwa binafsi wa taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za Serikali kwa mujibu wa sera za uendeshaji wa taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za Serikali.

3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo- Tafsiri.

"Afisa Masuuli" maana yake ni afisa masuuli aliyeteuliwa chini ya masharti ya Sheria ya Fedha za Umma;

"mamlaka ya kuidhinisha" maana yake ni Afisa Masuuli, Bodi ya Tenda ya Wizara, Bodi ya Tenda ya Shirika na Bodi ya Tenda ya Mkoa;

"Afisa aliyeidhinishwa" maana yake mtu aliyeteuliwa kuwa afisa aliyeidhinishwa chini ya Sheria hii;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Manunuzi na Uuzaji wa mali za Serikali ilioanzishwa chini ya kifungu cha 5 cha Sheria hii;

"Zabuni" maana yake ni ombi la kutowa au kupata kazi, huduma or usambazaji au yote yaliotajwa kwa ujumla wake katika zubuni, ikijumuisha sifa za awali pale itakapotumika;

"Mzabuni" maana yake ni mtu au taasisi inayotaka kushiriki, au inashiriki katika manunuzi au taratibu za uuzaji wa mali za serikali;

"Nyaraka za zabuni" maana yake ni nyaraka zinazotumika kwenye zabuni;

"Hati ya zabuni" maana yake ni tangazo lolote la zabuni ambalo wazabuni wenye sifa wanaalikwa kuwasilisha kwa maandishi bei zao kwa ajili ya kutoa au kupata kazi, huduma na kusambaza, au mjumuisho wa vyote hivyo katika manunuzi na uuzaji wa mali;

"ushindani wa kuchagua" maana yake ni njia ya manunuzi ambayo inatumika kwa kuchagua idadi ndogo ya washauri elekizi au watoa huduma walioalikwa baada ya kufanyiwa uchambuzi wa awali wa sifa zao na taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kwa kushindana miongoni mwao kwa misingi ya ubora na gharama baada ya tathmini ya awali;

"Mamlaka yenye uwezo" maana yake ni afisi ya Serikali ambayo ina mamlaka kisheria kufanya kazi zilizotajwa;

"Huduma za ushauri" maana yake ni huduma ya kutumia ubunifu wa akili au ushauri unaotolewa na mzabuni mwenye ujuzi na sifa katika sekta

husika au fani husika, ikijumuisha usanifu wa michoro au usimamizi, uhasibu, ukaguzi, huduma za fedha, huduma za manunuzi, mafunzo na huduma za kujenga uwezo, ushauri wa uongozi, mafunzo ya sera na ushauri, na usaidizi wa mabadiliko ya kitaasisi;

"Mshauri elekezi" maana yake ni mtu au taasisi, kampuni, shirika, jumuiya au ubiya unaotoa huduma za ushauri elekezi kwa taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

"Mkataba" maana yake ni makubaliano baina ya taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za Serikali na mtoaji, yaliyotokana na maombi husika ya zabuni na manunuzi yaliyothibitishwa au utaratibu wa kuuza uliofanywa kwa mujibu wa maamuzi yaliyotolewa na Bodi ya Zabuni au mamlaka husika;

"Mkandarasi" maana yake mjenzi kama alivyoelezwa ndani ya Sheria hii;

"Kamishna" maana yake Kamishna wa Idara kama ilivyoelezwa katika Sheria hii;

"kosa la rushwa" inajumuisha kutoa, kupewa, kupokea, kushawishi kitu cha thamani ambacho kitapelekea mtumishi wa umma katika manunuzi au uuzaji wa mali za Seikali, au katika utekelezaji wa mkataba;

"uuzaji" maana yake ni uuzaji wa mali za serikali ikijumuisha ubunifu na haki miliki, msaada na haki nyengine yoyote ya taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kwa njia yoyote ikijumuisha, kuuza, kukodisha, kukodi, ubiya, mnada au njia nyengine kati ya hiyo;

"taratibu za uuzaji" maana yake ni hatua inayochukuliwa katika utaratibu wa uuzaji, unaojumuisha kupanga, kuchugua taratibu za kufuatwa, kuchanganua maombi ya zabuni, kuchunguza na kutathmini maombi hayo na kubariki mkataba;

"dharura" maana yake ni mazingira ambayo ni ya haraka ambayo hayakutarajiwa na hayakusababishwa na kitendo cha ucheleweshaji.

"hali ya dharura" maana yake ni mazingira ya haraka ambayo hayakutarajiwa au hali ambayo haikusababishwa na kuitendo cha uchelewashaji ambapo -

(a) Zanzibar ipo katika hali hatarishi au imeathirika kwa janga, vita au janga la kimaumbile;

(b) maisha au hali ya maisha au mazingira ambayo yanaweza kuharibika sana;

(c) hali au ubora wa bidhaa, vifaa, majengo au mtaji unaomilikwa na mtaji wa bidhaa zipo katika hali mbaya ya kuharibika isipokuwa kwa hatua za haraka na za lazima zinahitajika kuchukuliwa ili kuzihifadhi bidhaa hizo katika thamani yake au ziweze kutumika;

(d) mradi wa kitega uchumi umechelewa sana kutokana na kukosekana kwa kitu kidogo;

(e) mpango wa Serikali utachelewa; au

(f) utaharibika isipokuwa manunuzi yatafanywa ndani ya muda unaohitajika;

"Mzabuni wa Kigeni" maana yake ni mzabuni ambaye biashara yake haijasajiliwa Zanzibar;

"matendo ya udanganyifu" inajumuisha udanganyifu wa kitu, ili kushawishi utaratibu wa manunuzi na uuzaji wa mali za serikali au utekelezaji wa mkataba kwa hasara kwa taasisi ya umma, na ikujumuisha kujiingiza katika vitendo viovu miongoni mwa wazabuni kabla au baada ya uwasilishaji wa zabuni kwa lengo la kutoa bei ya zabuni kwa mzabuni ambaye hana sifa na kukiuka taratibu za manunuzi na uuzaji wa mali za Seikali kwa taasisi kwa lengo la kujinufaisha kwa kufanya manununi yasio huru na ushindani;

"Maghala ya Serikali" maana yake ni ghala lolote lililowekwa bidhaa au huduma kwa taasisi za Serikali;

"Miongozo" maana yake ni malelekezo au miongozo inayotolewa na Mamlaka ilioanzishwa chini ya Sheria hii;

"Taasisi inayojitegemea" maana yake ni taasisi ya Serikali au Idara yenye kifungu chake cha matumizi katika bajeti ya Serikali;

"Viwango vinavyokubalika" maana yake ni viwango vilivyoelezwa na kukubalika kimataifa kwa mtoa huduma wa kimataifa, taasisi za Kitaalamu katika fani husika na ikijumuisha njia bora iliyozoeleka;

"Orodha ya Wazabuni" maana yake ni mzabuni aliyesajiliwa na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na mambo ya fedha;

"Mzabuni wa Zanzibar" maana yake ni mzabuni aliyesajiliwa Zanzibar na inamilikiwa na kuendeshwa na wanzanzibari;

"Huduma zisizokuwa za ushauri elekezi" maana yake ni huduma za kiujuzi au zisizokuwa za ujuzi ambazo sio huduma za ushauri elekezi na kujumuisha usafi, ulinzi, matengenezo na huduma za ukarabati;

"Mashirika ya Umma" maana yake ni-

(i) taasisi zilizoanzishwa kwa sharia;

(ii) Shirika lolote lililosajiwa chini ya Sheria za Makampuni ambapo si chini ya asilimia hamsini ya mtaji wa hisa unamilikiwa na Serikali au Sheria nyengine, au ikiwa Kampuni yenye ukomo kwa dhamana, pale ambapo Serikali inamiliki asilimia hamsini au zaidi ya dhamana ya kampuni; au

(iii) Kampuni yoyote, Bodi ya utawala, jumuiya au Bodi zilizoanzishwa kisheria ambazo Serikali ina hisa nyingi au inadhibiti riba;

"Mlipaji Mkuu" maana yake ni Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na mambo ya fedha na inajumuisha Mafisa wanaofanya kazi chini ya mamlaka ya Mlipaji Mkuu;

"Uchambuzi wa awali" maana yake ni utaratibu ulioweka wa kuchunguza kuhakikisha kwamba mialiko ya zabuni inawafikia wazabuni husika;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Barabara la Mapinduzi;

"Uchambuzi baada ya zabuni" maana yake ni utaratibu rasmi unaotumiwa baada ya zabuni kufanyiwa tathmini kabla ya kupewa mkataba, kuangalia kama mzabuni aliyeshinda kama ana uzowefu, uwezo na vitendea kazi kwa ajili kutekeleza mkataba kikamilifu;

"Manunuzi" maana yake kupata kwa njia kununua, ukodishwaji, kukodisha, kuajiri, kuruhusu, upangishaji, ubiya au njia nyengine yoyote ya mkataba ya aina yoyote ya kazi, huduma au usambazaji au yote kwa pamoja;

"Ubao wa matangazo ya zabuni" maana yake ni ubao wa matangazo ya zabuni ya taasisi za Serikali ambazo unatumika kuonesha matangazo ya zabuni zinayohitajika kutangazwa chini ya Sheria hii na Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii kuonesha taarifa nyenginezo zinazohusiana na manunuzi na shughuli za uuzaji kwa taasisi za umma;

"Kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za Serikali" maana yake ni Kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za Serikali katika taasisi chenye kuhusika na utekelezaji wa manunuzi na uuzaji wa mali za Serikali;

"Wakala wa manunuzi" maana yake ni mtu au taasisi yenye utaalamu wa manunuzi ambayo inafanyakazi kwa niaba ya taasisi nyengine inayojulikana kama muajiri wake katika kushughulika na mtu wa tatu katika mambo yanayohusiana na manunuzi;

"Taratibu za Manunuzi" maana yake ni hatua za mafanikio katika utaratibu wa manunuzi ikijumuisha mipango, njia itakayotumika, vipimo vya kushajihisha bei kutoka kwa wazabuni, kuangalia na kutathmini bei hizo na kumpata mshindi na kusimamia mkataba;

"Mtaalamu wa Manunuzi" maana yake ni mtu ambaye ni mtaalamu katika fani ya manunuzi, kazi au kuitwa katika maswala ya manunuzi kwa kuingia moja kwa moja au kinyume chake, ambaye ana taaluma na uzowefu wa kushughulika na manunuzi au ambaye amethibitishwa au amesajiliwa na Bodi ya Wataalamu wa Manunuzi;

"Taasisi za manunuzi na uuzaji wa mali za Serikali" maana yake ni-

(a) Wizara au Idara ya Serikali;

(b) Serikali za Mikoa;

(c) Halmashauri za Wilaya;

(d) Taasisi zinazojitegemea zilizoanzishwa na sheria;

(e) Kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria za Makampuni ambayo Serikali au taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za umma-

(i) ina idadi kubwa ya wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa kampuni;

(ii) inastahiki kura ya veto na inaongoza zaidi ya asilimia hamsini ya kura ambazo zitapigwa katika mkutano mkuu wa kampuni;

(iii) inadhibiti zaidi ya asilimia hamsini ya hisa zilizotolewa na kampuni, isipokuwa hisa zilizotolewa kama ni mtaji ambazo hazina haki ya kuchukuliwa kushiriki kinyume na zile ambazo kiwango chake kimetajwa katika mgawano wa faida au mtaji; na

(f) taasisi yeyote isiyokuwa ya Serikali ambayo masharti ya kifungu cha 2(1)(d) cha Sheria hii yanatumika na inajumuisha-

(i) Kamisheni iliyoanzishwa na sheria;

(ii) Chuo Kikuu cha Taifa na vyuo vya taasisi za Serikali vilivyoanzishwa na sharia;

(iii) Taasisi nyengine yoyote ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kama itakavyoelezwa na Waziri;

"Mzabuni" maana yake ni mtu au taasisi ikijumuisha mshaurielekezi, mkandarasi, mfanyabiashara aliyeruhusiwa na mamlaka husika kufanya biashara;

"Mali za Serikali" maana yake ni mali yoyote inayoshikika au isiyoshikika inayomilikiwa na serikali au taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali, ikujumuisha mali zinazoonekana, hisa, hisa za muwekezaji, ardhi, isipokuwa ardhi iliyopo chini ya dhamana ya Waziri anayehusika na ardhi au ardhi inayomilikwa na mamlaka ya mkoa au ardhi ya serikali iliyopatikana kwa mujibu wa sharia;

"Fedha za umma" maana yake ni fedha ambazo zinapatikana kupitia taratibu za kibajeti ikiwemo, Mfuko Mkuu wa Hazina, ruzuku na mikopo ambazo zimewekwa katika taasisi za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali ambazo zimetolewa na wahisani na mapato yanayopatikana kutoka kwenye taasisi za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

"Afisa wa Serikali" maana yake ni-

(a) mtu yeyote mwenyedhamana au anayefanyakazi katika afisi za Serikali;

(b) mtu anayemiliki au anayefanyakazi katika ofisi ya Waziri;

(c) mfanyakazi yeyote wa taasisi za serikali kama ilivyoelezwa katika tafsiri taasisi zinazojitegemea au idara za Serikali;

(d) mtu yeyote anayefanya majadiliano au inajihusisha na mikataba ya serikali au miongozo ya mikataba ya serikali kwa niaba ya taasisi ya umma;

(e) mtu ambaye ni mshauri elekezi kwenye taasisi za umma;

"Huduma" maana yake ni kitu chochote cha manunuzi au uuzaji kisichokuwa kazi au usambazaji, ikijumuisha fani za ujuzi na zisizokuwa za ujuzi na huduma za kibiashara pamoja usambazaji na kazi ambazo zimejitokeza, ambazo hazitozidi thamani ya huduma hiyo;

"Nyaraka za zabuni" maana yake ni nyaraka za zabuni au nyaraka zozote zile zinazowataka wazabuni kushirika katika mchakato wa manunuzi au uuzaji wa mali za serikali na ikijumuisha nyaraka za kuwalika wazubuni maalumu kushiriki katika zabuni na nyaraka nyengine za zabuni;

"Sifa" maana yake sifa ya kitu kinachotaka kununuliwa au kuondoshwa kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa vilivyokubalika na kuthibitishwa na Mamlaka, baada ya mashauriano na Bodi ya viwango, au jumuiya nyenginezo zinazohusiana na biashara na utaalamu, matumizi yake ni lazima yakuwepo katika kila zabuni;

"Bidhaa" maana yake ni bidhaa, malighafi, vifaa, mifugo,mali, ardhi au kitu chochote cha aina yeyote na chenye yabisi, vimiminika, au mfumo wa gesi au katika wa kieloktroniki, ubunifu na haki za umiliki na vile vile kazi au huduma zilizojitokeza katika bidhaa pale ambapo thamani ya kazi au huduma hazidi thamani ya bidhaa;

"Zabuni" maana yake ni bei, pendekezo au nyaraka za bazuni zilizofanywa na mzabuni, mkandarasi au mshaurielekezi kuhusiana na maombi ya taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

"Hadidu rejea" maana yake ni maelezo yanayotolewa na kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali yanayotoa ufanunuzi juu ya malengo, mwelekeo wa kazi, ikiwemo ambapo wapi inatakiwa kutumika;

"Uharaka" haitohusika na mazingira yafutayo-

(a) iwe imekadiriwa na kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

(b) iwe ni matokeo ambayo hayakupangwa;

(c) iwe ni matokeo ya kuchelewa kwa kitengo cha mnunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

"Idara inayotumia" maana yake Idara yoyote, Kitengo, Tawi au Taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serekali ikiwemo vitengo vya mradi vinavyofanya kazi chini ya Mamlaka ya manunuzi na uuzaji wa Mali za Serikali, ambayo itaanzisha mahitaji ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali na kuwa mtumiaji wa mahitaji;

"Kazi" maana yake ni kazi yoyote inayohusiana na ujenzi, mabadiliko ya ujenzi, ubomoaji, ukarabati, matengenezo ya jengo au umbile la jengo, juu ya jengo au chini, juu na chini ya maji, ikiwemo matayarisho, kuchimbua, kusimamisha jengo, kuuanganisha, uwekaji, majaribio, na kazi yoyote ya mitambo, vifaa au zana, mapambo, na umaliziaji wa kazi za miradi mikubwa, umiliki wa majengo na utekelezaji wa Miradi, uendeshaji wa majengo na uhamishaji wa miradi, au uandaaji wa kazi zinazohusiana, au utaratibu mwengine wowote wa binafsi na umma, utaratibu wowote wa ubia ambao wa umma na binafsi, au kazi za maendeleo za pamoja, au ambazo zitajumuisha uongozi, matengenezo, majaribio, kazi na mafunzo vilevile bidhaa, huduma au tukio la kazi ambapo thamani ya bidhaa au huduma haitozidi thamani ya kazi.

Majukumu ya Kimataifa.

4.-(1) Pale ambapo sheria hii itapingana na majukumu ya Serikali ya Mapinguzi Zanzibar yaliomo katika makubuliano na nchi moja au zaidi au kinyume na jumuiya za kimataifa, masharti ya makubaliano yatakuwa na nguvu kuliko Sheria hii.

(2) Pale ambapo makubaliano yaliyoelezwa katika kifungu (1) kinataka kuwepo na upendeleo kwa wazabuni ndani na wakaazi, taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali uhakikishe kwamba kuwepo kwa upendeleo huo unaelezwa wazi katika nyaraka za zabuni.

(3) Pale ambapo mikopo baina ya nchi na nchi au mapatano ya msaada yameweka masharti kwamba mzabuni lazima awe anatoka nchi yenye kufadhili, manunuzi yafanywe kwa mujibu wa Sheria hii.

(4) Bila ya kuathiri kifungu kidogo (3), pale inapotokea mgongano baina ya Sheria hii, kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii au miongozo iliyotolewa na Mamlaka na masharti yaliyotolewa na wafadhili wa fedha, masharti yaliyotolewa na wafadhili ndiyo yatakayofuatwa katika manunuzi yanayotumia fedha za wafadhili.

SEHEMU YA PILI
MAMLAKA YA UNUNUZI NA UUZAJI WA MALI ZA SERIKALI

Kuanzishwa kwa Mamlaka.

5.-(1) Kunaanzishwa Mamlaka ya Ununuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali ambayo itakuwa ni chombo cha Serikali kinachojitegemea.

(2) Mamlaka itakuwa-

(a) chombo chenye kujitegemea endelevu na chenye mhuri wake;

(b) chenye uwezo wa kushitaki na kushitakiwa;

(c) chenye uwezo wa kukopa fedha, kupata na kuuza mali kwa jina lake; na

(d) kufanya jambo lolote la kihalali ambalo chombo kujitegemea kinaweza kufanya.

(3) Matumizi ya muhuri wa mamalaka yaliyotumika kwenye nyaraka yoyote yatatambuliwa kwamba ni halalai iwapo kutakuwa na saini ya mkurugenzi mtendaji au mtu mwengine yeyote wa mammlaka ambaye ameidhinishwa na mkurugenzi mtendaji.

(4) Nyaraka yoyoteitakayotolewa na Mamlaka ni lazima iwekwe muhuri wake na itakuwa halali kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, itatambulika kama ni nyaraka ya mamlaka na itachukuliwa kama ushahidi ambao hautahitaji ithibati nyengine yoyote.

Majukumu ya Mamlaka

6. Majukumu ya Mamlaka ni-

(a) kuhakikisha usawa, ushindani, uwazi, bila ya ubaguzi na thamani ya fedha kwa ununuzi na uuzaji unazingatia viwango na uhalisia;

(b) kushauri Serikali Kuu, serikali za mitaa, mashirika na vyombo vyote vinavyojihusisha na ununuzi na uuzaji kuhusiana na sera, mifumo na uzoefu na pale inapoonekana inafaa kutumika kwa pamoja;

(c) kuweka viwango vya mifumo ya umma juu ya ununuzi na uuzaji Zanzibar;

(d) kusimamia utekelezaji wa masharti ya ununuzi na uuzaji kwa vyombo husika;

(e) kujenga uwezo wa uweledi wa ununuzi na uuzaji Zanzibar; na

(f) kuhifadhi daftari la watoa huduma za ununuzi na uuzaji pamoja na taaluma za ununuzi.

Kazi za Mamlaka.

7. Kazi za Mamlaka zitakuwa ni-

(a) kushauri Serikali kuu, serikali za mitaa na vyombo vyengine vinavyojihusisha na uunuzi na uuzaji juuya sera, misingi na uzoefu ya manunuzi ya umma;

(b) kusimamia na kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa mfumo wa ununuzi na uuzaji wa umma Zanzibar na kushauri mabadiliko yafaayo;

(c) kushauri mamlaka husika juu ya viwango vya manunuzi vinavyohusiana na taaluma na mafunzo na uweledi na masharti stahiki;

(d) kuandaa, kuweka taarifa mpya na kuzisambaza nyaraka za zabuni, fomu za utaratibu wa zabuni na nyaraka nyengine yoyote itakayowasilishwa kwa ajili ya ununuzi na uuzaji;

(e) kuhakikisha kwamba marekebisho yanayofanywa katika fomu za zabuni hayafanyiki mpaka kuwe na ruhusaya maandishi itakayotolewa na Mamlaka;

(f) kutoa miongozo kwa mujibu wa mashati ya Sheria hii;

(g) kuratibu na kuthibiti mfumo wa uchapaji wa taarifa za data juu ya fursa za ununuzi na uuzaji wa umma, mshindi wa zabuni na taarifa nyengine yoyote kwa maslahi ya umma kama mamlaka itakavyoona inafaa;

(h) kuhifadhi daftari la kazi, huduma na wasambazaji;

(i) kufanya ukaguzi wa muda wa nyaraka na mwenendo wa uendeshaji wa vyombo vinavyojihusisha na uuzaji na ununuzi ili kuhakikisha matumizi sahihi ya Sheria hii yanatekelezwa;

(j) Taasisi-

(i) ukaguzi wa hesabu za fedha za ununuzi na uuzaji wakati wa matayarisho ya zabuni;

(ii) mikataba imekaguliwa wakati wa kumchagua mtu au taasisi iliyoshinda zabuni husika; na

(iii) kufanya ukaguzi wa hesabu za fedha baada ya kumalizika mikataba kuhusiana na kitu chochote cha uuzaji na ununuzi kama itakavyohitajika;

(k) kufuata na kutekeleza viwango mahususi ambayo ni muhimu katika kufanikisha suala la ununuzi na uuzaji kwa taasisi husika;

(l) kuzingatia, kuandaa, kuanzisha, kuhifadhi mfumo wa kuweka kumbukumbu na teknolojia kwa upana wake;

(m) kukuza uweledi wa uwezo wa mikakati ya ununuzi na uuzaji kwa taasisi husika na maendeleo ya rasilimali watu;

(n) pale inapohitajika, kuamua gharama za kazi, huduma na usambazaji ambazo zinatumiwa na taasisi mbili au zaidi zinazojihusisha na ununuzi na uuzaji na kupitia upya gharama muda baada ya muda;

(o) kuanzisha na kuhifadhi siri za taasisi za kitaalamu zinazojihusisha na ununuzi na uuzaji kwa maslahi ya umma;

(p) kufanya tafiti za kitaifa na kimataifa zinazohusiana na ununuzi na uuzaji;

(q) kufanya kazi nyengine yoyote ambayo ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake; na

(r) kusimamia na kuhakikisha utekelezaji wa masharti ya Sheria hii, Kanuni na miongozo inatekelezwa kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Mamlaka inaweza kuingia mikataba na mtu mwengine kufanya ukaguzi wa fedha, uchunguzi na kuhakiki wa kazi za ununuzi.

(3) Mamlaka itatua mgogoro wowote utakaojitokeza kuhusiana na uelewa wa masharti ya Sheria hii kwa kufuata utaratibu utakaoelezwa na Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii.

Uwezo wa mamlaka.

8.-(1) Katika kutekeleza kazi zake za usimamizi, Mamlaka itakuwa na uwezo wa-

(a) kuomba kupatiwa taarifa yoyote, nyaraka , kumbukumbu na ripoti kuhusiana na mchakato wa ununuzi na uuzaji wa mali za umma pale ambapo kuna ukiukwaji wa masharti hayo, uongozi mbovu au mgomo umejitokeza katika taasisi hizo;

(b) kiuta mashahidi kuwasilisha vitabu vya hesabu, mipango, nyaraka na kumuuliza masuali shahidi na kulisha kiapo wahusika;

(c) kutoza malipo ya uchuguzi au kuendesha uchunguzi kwa taasisi husika ya ununuzi na uuzaji pamoja na ripoti ya utekelezaji wa ukaguzi wa fedha;

(d) kuchunguza miamala ya uuzaji na ununuzi kwa ajili ya kuhakikisha yanafuatamasharti ya zabuni yaliyopewa taasisi husika;

(e) kusikiliza malalamiko yoyote ya uuzaji na ununuzi yaliyofanywa na taasisi yoyote kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(f) kumsimamisha mtoaji huduma za uuzaji na ununuzi wa mali za serikali kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

(2) Kwa madhumni ya kufanya ukaguzi wa uuzaji na ununuzi au utekelezaji wa uchunguzi unafanyika sahihi, Mkurugenzi Mtendaji anaweza kwa maandishi-

(a) kumuidhinisha afisa yeyote wa Mamlaka; au

(b) kuteua mtu yeyote kuwa afisa muidhinishaji kuingia sehemu yoyote inayojihusisha na uuzaji na ununuzi kwa ajili ya ukaguzi wakati wowote unaofaa na kukagua na kufanya uchunguzi kwa ajili ya kukusanya taarifa muhimu.

(3) Endapo afisa wa mamlaka au mtu aliyeidhinishwa amezuiwa kuingia kwa ajili ya ukaguzi kwa mujibuy wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Hakimu anaweza baada ya kupokea ombi kutoka Mamlaka kutoa hati ya kukamatwa na kumuamuru afisa wa Polisi kuingia eneo hilo kwa nguvu zinazokubalika kwa ajili ya ukaguzi na kupata taarifa muhimu.

Hatua za mapendekezo kwa Mamlaka.

9.-(1) Endapo itatokea uvunjifu wa masharti ya Sheria hii, kanuni au miongozo iliyoandaliwa kwa mujibu wa Sheria hii, Mamlaka inaweza-

(a) kuitaka taasisi husika inayojishughulisha na uuzaji na ununuzi kufanya masahihisho kwa kadri inavyohitajika na katika mazingira ya kusahihisha kosa; au

(b) kushauri kwa mamlka husika-

(i) kumsimamisha afisa aliyehusika na kosa hilo;

(ii) kumuondosha kiongozi wa kitengo cha uuzaji na ununuzi au Mwenyekiti wa Bodi ya Zabuni, kama itakavyohitajika;

(iii) kupendekeza kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa Afisa Masuuli;

(iv) kuhamisha kwa muda kazi za uuzaji na ununuzi kwa wakala wa uuzaji na ununuzi.

(2) Mamlaka inayohusika itatoa majibu kwa maamdishi juu ya mapendekezo ya Mamlaka kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1)(b) cha kifungu hiki, ndani ya kipindi kilichoainishwa na Kanuni iliyoandaliwa kwa mujibu wa Sheria hii.

(3) Endapo mamlaka inayohusika imekataa kutekeleza mapendekezo ya Mamlaka chini ya kifungu kidogo cha (1)(b) cha kifungu hiki, Mamlaka italazimika-

(a) kuwasiliana na wakala msimamizi kwa kumpelekea mapendekezo yao, na nyaraka nyenginezo kwa kumtaka achukuwe hatua stahiki;

(b) kuomba kuchukuliwa kwa hatua yoyote kwa mamlaka husika kwa mujibu wa uwezo waliopewa.

(4) Mamlaka husika italazimika kujibu kwa maandishi mapendekezo ya mamlaka katika kipindi kilichoainishwa na Kanuni zilizoandaliwa chini ya Sheria hii na kuelezea kwa kifupi hatua zilizochukuliwa kwa mujibu wa mapendekezo au kutoa ufafanuzi ikiwa hakuna hatua iliyochukuliwa.

(5) Mamlaka italazimika kujumuisha taarifa zifuatazo katika ripoti ya tathimini ya mwaka kama zifuatazo-

(a) mambo yaliyojitokeza katika ukaguzi wa hesabu na malalamiko waliyoyachunguza;

(b) hatua ya masahihisho zilizopendekezwa kwa kila jambo;

(c) majibu juu ya-

(i) Mamlaka husika stahiki;

(ii) Sheria zinazohusiana na utekelezaji wa uuzaji na ununuzi na wakala msimamizi;

(d) na hatua nyengine yoyote iliyochukuliwa.

Kuanzishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi.

10.-(1) Kunaanzishwa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ambayo itatekeleza kazi na uwezo wake kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Bodi itaundwa na wajumbe wafuatao-

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mlipaji Mkuu wa Serikali;

(c) Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka;

(d) Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu;

(e) Mtu moja kutoka Jumuiya ya Wahasibu na Wakaguzi ya Zanzibar;

(f) Mtu mmoja kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara na Viwanda ya Zanzibar;

(g) Si zaidi ya wajumbe wengine watatu ambao watateuliwa na Waziri.

(3) Mbali ya Wajumbe kwa nafasi zao, wajumbe wengine watateuliwa na Waziri baada ya kushauriana na Taasisi husika ikizingatiwa kwamba Waziri atazingatia jinsia wakati wa uteuzi wa wajumbe hao.

(4) Wakili wa Serikali anayefanya kazi zake Wizara ya fedha atakuwa Katibu wa Bodi.

Sifa za Mwenyekiti.

11. Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mwenyekiti ikiwa mtu huyo-

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza ya ununuzi na usambazaji, uongozi, uhandisi, uchumi, sheria au fani nyengine yoyote inayofanana kutoka katika chuo kinachotambulika;

(c) ana uzoefu wa kazi angalau kwa miaka kumi na tano na angalau miaka kumi ya uongozi au utumishi wa umma; na

(d) ana heshimika kutokana na mwenendo wake mzuri kwa Serikali na jamii kwa ujumla.

Kazi za Bodi.

12.-(1) Bodi itakuwa na wajibu wa kutoa miongozo ya ujumla na usimamizi wa kazi za Mamlaka.

(2) Bila kuathiri madhumuni ya ujumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Bodi ina wajibu wa-

(a) kuangalia utendaji wa jumla wa Mamlaka;

(b) kuishauri Serikali juu ya sera ya ununuzi na mipango mikakati;

(c) kusimamia na kuangalia utendaji kazi wa Mamlaka;

(d) kuangalia kufuatwa kwa masharti ya sharia yanayohusiana na ununzi na uuzaji wa mali za Serikali;

(e) kuamua juu ya uteuzi wa watumishi wa Mamlaka na kuwapangia kazi na majukumu pamoja na kuweka vigezo na masharti ya

kazi ikijumuisha upandishaji vyeo, hatua za kinidhamu na kufukuza kazi;

(f) kupanga mikakati, mipango ya kazi na matarajio mengine ya utendaji kwa kila Idara ya Mamlaka; na

(g) kutekeleza kazi nyengine yoyote iliyopewa kwa mujibu wa Sheria ambayo ni muhimu katika kufikia malengo ya kuanzishwa kwa Mamlaka.

Muda wa Bodi.

13. Wajumbe wa Bodi isipokuwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, watatumikia kwa kipindi cha miaka mitatu isipokuwa kama uteuzi wao utatenguliwa au kusita kwa namna nyengine yoyote, na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Vikao vya Bodi.

14.-(1) Bodi itafanya vikao vyake vya kawaida angalau mara moja kwa kila kipindi cha miezi mitatu na inaweza kukutana muda wowote katika utekelezaji wa kazi zake lakini vikao vya dharura hakitozidi kimoja ndani ya kipindi cha miezi miwili.

(2) Vikao vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti au ikiwa hayupo, na Makamo Mwenyekiti na ikiwa Mwenyeki na Makamo Mwenyekiti wote hayapo, wajumbe waliopo watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuangoza kikao hicho.

(3) Akidi ya kikao cha Bodi itakuwa ni wajumbe wanne, isipokuwa kama mjumbe ameeleza mamlahi juu ya hoja au jambo liliyopo mbele ya Bodi, mjumbe huyo hatohisabiwa kujumushwa katika akidi kuhusiana na hoja au jambo hilo.

(4) Mjumbe baada ya kupata ajenda ya kikao cha Bodi, au baada ya kuapata taarifa ya jambo litakalojadiliwa na Bodi, atalazimika-

(a) kujaza fomu ya tamko kama ilivyoelezwa katika Jadweli la kwanza la Sheria hii, akionesha kama anamaslahi au anakusudia kuwa na maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo katika ajenda hiyo au jambo linalohitaji kuzingatiwa na kutolewa maamuzi na Bodi; na

(b) endapo kama atakuwa na maslahi hayo, hatoshiriki katika majadiliano au kufanya maamuzi ya Bodi kuhusiana na ajenda au jambo hilo.

(5) Maamuzi ya Bodi yatafanywa kwa wingi wa kura za Wajumbe na endapo itatokea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

(6) Kumbukumbu za kikao cha Bodi zitathibitishwa katika kakao cha Bodi kinachofuata.

(7) Bodi itaweka utaratibu wa kuendesha vikao vyake katika kutekeleza kazi zake.

Kamati za Bodi.

15.-(1) Bodi inaweza kuanzisha Kamati ya Kupitia Malalamiko ambayo itashughulikia malalamiko kutoka kwa watoa huduma na mtu mwengine yeyote, yanakayohusiana na kazi za ununzi na uuzaji wa taasisi za manunuzi na uuzaji.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Bodi inaweza kuanzisha kamati nyengine yoyote ambayo itaona ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Mamlaka.

(3) Bodi itaamua muundo, masharti ya utendaji kazi na vigezo vyengine na utendaji wa kamati.

Kukasimu kazi na uwezo.

16.-(1) Bodi inaweza, kwa hati maalumu ya maandishi, kukasimu kwa kamati au Mkurugenzi Mtendaji, kazi yoyote au uwezo wake isipokuwa-

(a) kazi ya kusimamia na kutoa taarifa ya utekelezaji wa mifumo ya uuzaji na ununuzi ya Zanzibar na kushauri marekebisho stahiki;

(b) kazi ya kushauri mamlaka husika kwa ajili ya kukuza na kuendeleza viwango vya mafunzo, viwango vya uweledi na masharti stahiki ya uuzaji na ununuzi wa mali za serikali;

(c) kazi ya kutayarisha na kutoa nyaraka zilizothibitishwa za zabuni, fomu za miongozo na nyaraka yoyote iliyowasilishwa kwa ajili ya ununuzi na uuzaji kutoka taasisi husika;

(d) kazi ya kutoa miongozo;

(e) kazi ya kuanzisha-

(i) ukaguzi wa hesabu wakati wa matayarisho ya zabuni;

(ii) ukaguzi wa mikataba wakati wa utekelezaji wa zabuni ya mshindi;

(iii) kufanya ukaguzi baada ya kumalizika mkataba kuhusiana na ununuzi na uuzaji kama itakavyohitajika;

(f) uwezo wa kusikiliza malalamiko kutoka katika taasisi za ununuzi na uuzaji, wasambazaji na chombo chochote au watu wanaojishughulisha na uuzaji au ununuzi; na

(g) uwezo wa kumsimamisha mtoa huduma za uuzaji na ununuzi wa umma.

(2) Mtu yeyote aliyekasimiwa kazi au uwezo anawajibika kufuata masharti, vigezo na maelekezo na miongozo itakayotolwa na Bodi.

(3) Mtu atakayekuwa hakuridhika na maamuzi yaliyotolewa chini ya kifungu hiki anaweza kukata rufaa kwa Bodi ndani ya kipindi cha miezi mitatu kuanzia tarehe ya uamuzi huo.

Kusita wa utumishi wa Bodi.

17.-(1) Mamlaka ya uteuzi inaweza, wakati wowote kusitisha uteuzi wa mjumbe yeyote wa Bodi ikiwa-

(a) amefanya matumizi mabaya ya afisi;

(b) amechukuwa au kutoa rushwa;

(c) hana uwezo;

(d) hawezi kimwili au kiakili kutekeleza vyema kazi zake;

(e) ameshindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya sababu ya msingi;

(f) ametiwa hatiani kwa makosa ya kimaadili; au

(g) jambo jengine lolote.

(2) Mjumbe yeyote wa Bodi anaweza kujiuzulu kwa kuitaarifu mamlaka ya uteuzi angalau si chini ya mwezi mmoja taarifa yake kwa maandishi.

Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

18.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ambaye atateuliwa na Rais kwa vigezo na masharti kama yatakavyoainishwa kwenye hati yake ya uteuzi.

(2) Mtu atafaa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji ikiwa mtu huyo-

(a) ni mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza ya ununuzi na usambazaji, usimamizi wa mali, uhandisi, fedha, uchumi, sheria au fani nyengine yoyote iliyofanana na hizo kutoka katika chuo kinachotambulika; na

(c) ana uzoefu wa kufanya kazi wa kipindi cha miaka kumi na tano, na miaka kumi ameitumia kwenye masuala ya ununuzi au uongozi au utumishi wa umma.

(3) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa na wajibu wa kutekeleza kazi za kila siku za Mamlaka, na atakuwa na wajibu wa-

(a) kusimamia uongozi na utendaji wa Mamlaka;

(b) kusimamia fedha, rasilimali, mali na kazi za Mamlaka;

(c) usimamizi wa muundo, maafisa na wafanyakazi wa Mamlaka; na

(d) kukuza mafunzo na kutoa adhabu za kinidham kwa wafanyakazi wa Mamlaka.

(4) Mkurugenzi Mtendaji hatotakiwa kujihusisha na biashara yoyote, ujuzi, kazi au ajira yenye malipo sehemu nyengine.

Watumishi wengine wa Mamlaka.

19.-(1) Bodi itateua watumishi wengine wa Mamlaka kama itakavyohitajika kwa ajili ya utekelezaji kazi za Mamlaka kwa vigezo na masharti ya utumishi kama itakavyoamuliwa na Mamlaka.

(2) Mamlaka inaweza ili kurahisisha utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii, kuanzisha idara, kitengo au sehemu itakayoongozwa na mkuu na watumishi wengine kama itakavyoamuliwa na Bodi.

Fedha za Mamlaka.

20.-(1) Fedha za Mamlaka zitajumuisha-

(a) fedha zitakzopitishwa na Baraza la Wawakilishi kwa madhumuni ya Mamlaka;

(b) mikopo au zuruku itakayotolewa kwa Mamlaka kwa ajili ya kazi zake; na

(c) makusanyo yatakayopokewa kutoka katika huduma zinazotolewa na Mamlaka.

(2) Mamlaka inafungua akaunti ya Benki katika Benki itakayoidhinishwa na Bodi.

(3) Mwaka ya fedha wa Mamlaka utakuwa ni sawa na mwaka wa fedha wa Serikali.

Mpango wa utendajikazi na bajeti.

21.-(1) Mkurugenzi Mtendaji ataandaa sio zaidi ya miezi mitatu kabla ya kumalizika mwaka wa fedha, mpango wa kazi wa mwaka ambao utajumuisha makadirio ya matumizi kwa ajili ya mwaka wa fedha unaofuata, na kuwasilisha kwa Bodi.

(2) Mkurugenzi mtendaji anaweza wakati wowote kabla ya kumalizika mwaka wa fedha kuandaa na kuwasilisha bajeti ya ziada kwa ajili ya kuidhinishwa na Bodi.

(3) Hakuna matumizi yatakayotumika kutokana na fedha za Mamlaka isipokuwa matumizi hayo yameidhinishwa na Bodi katika makisio ya bajeti yake au bajeti ya ziada.

Hesabu na ukaguzi.

22.-(1) Mamlaka itawajibika kutunza vitabu vya hesabu na kumbukumbu nyenginezo za miamala yote.

(2) Hesabu za kila mwaka za Mamlaka pamoja na shughuli za ununuzi na uuzaji zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ripoti ya mwaka ya utekelezaji.

23.-(1) Mamlaka italazimika ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha, kuwasilisha kwa-

(a) Waziri taarifa ya utekelezaji wa mwaka wa kazi zilizotekelezwa katika mwaka huo itakayojumisha-

(i) taarifa ya fedha na mpango wa usimamizi;

(ii) tathmini ya uendeshaji wa mamlaka na taasisi zinazojihusisha na ununuzi na uuzaji; na

(iii) tarifa nyengine yoyote kama Bodi itakavyoelekeza; na

(b) kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali-

(i) taarifa ya hesabu ya fedha za Mamlaka kwa mwaka huo wa fedha;

(ii) taarifa ya tathmini iliyoelezwa katika aya (a) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(2) Waziri atawasilisha Baraza la Wawakililshi ripoti ya tahmini ya utemdaji kazi ndani ya miezi miwili au katika kikao kinachofuata, kutegemea kitakachotangulia.

(3) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha ripoti yake ya ukaguzi wa hesabu Baraza la Wawakilishi ndani ya miezi minne baada ya kumaliza ukaguzi wake.

Ukaguzi wa hesabu wa mkaguzi wa ndani.

24.-(1) Kwa kuongezea kazi nyengine yoyote waliopewa na Bodi au Mkurugenzi Mtendaji, mkuu wa mkaguzi wa ndani atakuwa na wajibu wa kufanya ukaguzi wa ndani kwa Mamlaka na atawasilisha ukaguzi huo kwa Mkurugenzi Mtendaji ripoti kila baada ya miezi mitatu ya mwaka wa fedha husika.

(2) Mkurugenzi Mtendaji atawasilisha ripoti zilizowasilishwa kwake kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kwa Bodi kwa ajili ya mazingatio katika kikao kinachofuata baada ya kupokea taarifa.

SEHEMU YA TATU
TAASISI ZA MANUNUZI NA UUZAJI WA MALI

Taasisi za manunuzi na uuzaji wa mali.

25. Kwa madhumuni ya Sheria hii, taasisi za manunuzi na uuzaji wa mali zitakuwa ni:-

(a) Afisa Masuuli;

(b) Bodi ya Zabuni;

(c) Kitengo cha Manunuzi na Uuzaji wa Mali; na

(d) Idara inayohusika.

Mamlaka ya taasisi za manunuzi na uuzaji wa mali.

26.-(1) Taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali itasimamia shughuli zote za manunuzi na uuzaji wa mali ndani ya mamlaka yake kwa mujibu wa Sheria hii, kanuni na miongozo itakayotolewa chini ya Sheria hii.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, Mlipaji Mkuu, kwa kila mwaka wa fedha atachaguwa wakala wa kufanya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali katika Mamlaka, isipokuwa kwa manunuzi madogo ambayo yatafanywa na Mamlaka.

Afisa Masuuli.

27.-(1) Afisa Masuuli wa taasisi za manunuzi na uuzaji wa mali atakuwa na majukumu ya jumla katika kutekeleza manunuzi na uuzaji wa mali za serikali katika taasisi za manunuzi na Zaidi ya hayo, atakuwa na majukumu ya-

(a) kuanzisha Bodi ya Zabuni kwa mujibu wa Sheria hii;

(b) kuteua wajumbe wa Bodi ya Zabuni na kuthibitishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali;

(c) kuagiza kuanzishwa kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali na kuajiri wafanyakazi wenye viwango;

(d) kutangaza nafasi za zabuni;

(e) kutangaza maamuzi ya mshindi wa zabuni;

(f) kuthibitisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

(g) kusaini mikataba kwa kazi za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kwa niaba ya taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za Serikali.

(h) kusikiliza malalamiko kutoka kwa wazabuni;

(i) kuwasilisha nakala za malalamiko na ripoti za matokeo ya uchunguzi kwa Mamlaka; na

(j) kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mkataba kwa aliyeshida unatekelezwa kwa mujibu wa taratibu na masharti ya mkataba.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo (1)(g) cha kifungu hiki, Afisa Masuuli hatoweza kusaini mkataba wa manunuzi kabla ya kuthibitishwa na Bodi ya Zabuni isipokuwa itakapotokea hali ya dharura ambayo Bodi ya Zabuni haiwezi kukutana na kuthibitisha manunuzi.

(3) Pale ambapo Afisa Masuuli amesaini Mkataba wa manunuzi kwa dharura kwa chini ya kifungu kidogo (2) ya kifungu hiki, Afisa Masuuli atalazimika-

(a) kuijuusha Bodi ya Zabuni juu ya Mkataba huo ndani ya siku saba za kazi tokea kusainiwa kwa Mkataba; na

(b) ndani ya siku kumi za kazi baada ya kusainiwa mkataba atawasilisha mkataba, kwa Mamlaka.

Bodi za Zabuni.

28.-(1) Kwa mujibu wa kifungu kidogo (2) cha kifungu hiki, Bodi ya Zabuni itaundwa na Wakuu wa Idara waliotajwa katika Jadweli la pili la Sheria hii.

(2) Wajumbe wa Bodi ya Zabuni watateuliwa na Afisa Masuuli na kuthibitishwa na Mlipaji Mkuu.

(3) Maafisa wafuatao wa taasisi za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali hawaruhusiwi kuteuliwa kuwa wajumbe wa Bodi ya Zabuni wa taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali-

(i) Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi; na

(ii) Wafanyakazi wa Idara ya ukaguzi wa ndani.

(4) Pale ambapo Afisa Masuuli anapoteua wajumbe wa Bodi ya Zabuni, kabla ya kuthibitisha uteuzi wao na Mlipaji Mkuu kwa mujibu wa kifungu kidogo (2) cha kifungu hiki, kumejitokeza hali ya dharura ambayo shughuli za manunuzi lazima zitekelezwe, Afisa Masuuli atafanya kazi kama Bodi ya Zabuni.

(5) Pale ambapo Afisa Masuuli anapofanya kazi za Bodi ya Zabuni chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, Afisa Masuuli atalazimika kuwasilisha taarifa ya manunuzi aliofanya kwa Mamlaka na nakala kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

(6) Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na uuzaji wa mali za serikali atahudhuria vikao vya Bodi ya Zabuni kwa ajili ya kutoa ufafanuzi kwa vitu vilivyowasilishwa katika Bodi ya Zabuni.

(7) Bodi ya Zabuni inaweza kuteua washauri kusaidia katika kutekeleza kazi zake.

(8) Afisa Masuuli atatakiwa kuiarifu Mamlaka juu ya muundo wa Bodi ya Zabuni na sifa za wajumbe wake sio zaidi ya siku kumi na nne tokea siku ya kuteuliwa.

(9) Wajumbe wa Bodi ya Zabuni watateuliwa kwa kuzingatia uwezo wao na ujuzi unaohitajika katika kutekeleza kazi za Bodi ya Zabuni.

(10) Muda wa Wajumbe wa Bodi ya Zabuni utakuwa ni miaka mitatu na mjumbe anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kimoja zaidi.

(11) Pale ambapo Mlipaji Mkuu atathibitisha kwamba haikuwa inafaa kutumia kifungu kidogo cha (10) cha kifungu hiki, Mlipaji Mkuu atasamehe yaliyofanywa na taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za Serikali kutokana na kutumia kifungu kidogo hicho.

Kazi za Bodi ya Zabuni.

29.-(1) Bodi ya Zabuni itakuwa na kazi zifuatazo-

(a) kupitia mapendekezo kutoka kitengo cha manunuzi na kuchaguwa mshindi wa zabuni;

(b) kuthibitisha kamati ya tathmini;

(c) kuthibitisha kamati ya kufanya mapatano;

(d) kuhakikisha kwamba kabla ya kuthibitisha, manunuzi yamefanywa kwa mujibu wa mpango wa manunuzi;

(e) kuthibitisha zabuni na nyaraka za mikataba;

(f) kazi zifuatazo kwa madhumuni ya uuzaji wa mali za serikali kwa taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

(g) kutathmini na kuhakiki mali za serikali zilizoorodheshwa na idara husika au Bodi ya ukaguzi kwa ajili ya kuondoshwa;

(h) kupelekea mali zilizoorodheshwa chini ya aya ya (g) kufanyiwa uthamini kwa mujibu wa kanuni zitakazotungwa chini ya sheria hii;

(i) kuthibitisha bei iliowekwa kwa ajili ya mali zinazotaka kuondoshwa;

(j) kuthibitisha taratibu za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

(k) kuhakikisha kuwa njia bora zinazohusiana na manunuzi na uuzaji wa mali za serikali zinafuatwa katika taasisi za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

(l) kuhakisha kwamba sheria hii inatekelezwa; na

(m) kushirikiana moja kwa moja na Mamlaka juu ya masuala ambayo yamo ndani ya mamlaka yake.

(2) Bodi ya Zabuni itatoa taarifa kuhusiana na kazi zilizotajwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki na kuwasilisha taarifa kwa Afisa Masuuli kwa kuthibitishwa.

Uwezo wa Bodi ya Zabuni.

30. Bodi ya zabuni-

(a) itaidhinisha-

(i) mapendekezo ya njia za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

(ii) nyaraka za zabuni kabla ya kutolewa;

(iii) taarifa ya tathmini ya zabuni kiufundi na fedha;

(iv) nyaraka za mikataba zinaendana na taarifa ya tathmini iliyothibitishwa; na

(v) marekebisho yeyote kwa aliyepewa mkataba;

(b) itapendekeza shughuli nyengine za manunuzi au kazi za uuzaji wa mali za serikali kwa Afisa Masuuli pale ambapo itahitajika; na

(c) kuidhinisha mikataba kwa mujibu wa taratibu za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kama itakavyojitokeza.

Kitengo cha Manunuzi na uuzaji wa mali.

31.-(1) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itaagiza kuanzishwa kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali chenye wafanyakazi wenye taaluma zinazohitajika.

(2) Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na uuzaji wa mali lazima awe na taaluma ya manunuzi.

Kazi za Kitengo cha Manunuzi na uuzaji wa mali za serikali.

32.-(1) Kitengo cha Manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kitakuwa na kazi zifuatazo-

(a) kusimamia kazi zote manunuzi na uuzaji wa mali za serikali katika taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali isipokuwa maamuzi na utoaji wa mkataba;

(b) kusaidia kazi za Bodi ya Zabuni;

(c) kutekeleza maamuzi ya Bodi ya Zabuni;

(d) kushirikiana moja kwa moja na Mamlaka katika mambo yaliyo katika mamlaka yake;

(e) kufanyakazi za sekreterieti ya Bodi ya Zabuni;

(f) kupanga mipango ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali za taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

(g) kupendekeza utaratibu wa manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

(h) kupendekeza wajumbe wa kamati ya tathmini na mapatano;

(i) kutayarisha na kupitia vigezo vitakavyotumika;

(j) kutayarisha nyaraka za zabuni;

(k) kutayarisha matangazo ya zabuni;

(l) kutoa nyaraka za zabuni;

(m) kuweka orodha ya wazubuni;

(n) kutayarisha nyaraka za mikataba na kutoa nyaraka za mikataba zilizothibitishwa;

(o) kuziweka na kuzihifadhi taarifa za utaratibu uliotumika katika manunuzi na uuzaji na uuzaji wa mali za serikali;

(p) kutayarisha taarifa za mwezi kwa ajili ya Bodi ya Zabuni;

(q) kuunganisha shughuli za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kwa idara zote ndani ya Wizara;

(r) kutayarisha taarifa nyengine yeyote ambazo zinaweza kuhitajika wakati wowote;

Uwezo wa Kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali.

33. Kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kitakuwa na uwezo wa-

(a) kupendekeza muundo wa kamati za tathmini na kamati ya mapatano, kwa ajili ya kuthibitishwa na Bodi ya Zabuni;

(b) kupokea ushauri binafsi ikiwa unahitajika katika kutekeleza kazi zake.

(c) kuhakikisha utekelezaji wa sheria hii, kanuni pamoja na miongozo iliyowekwa na sheria hii na njia bora;

(d) kusimamia maombi ya zabuni na upembuzi wa awali kwa kupeleka mapendekezo hayo katika Bodi ya Zabuni;

(e) kutoa ufafanuzi wa zabuni; na

(f) kupokea zabuni.

Kutokubaliana baina ya Bodi ya Zabuni na Kitengo cha Manaunuzi.

34.-(1) Pale ambapo Bodi ya Zabuni haitakubaliana na mapendekezo ya Kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali, Bodi ya Zabuni inaweza-

(a) kurejesha taarifa za manunuzi kwa Kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kwa ajili ya kufanyiwa mapitio na kuandika sababu zilizopelekea kutokubaliana; au

(b) kuomba ushauri huru kutoka kwa Mamlaka.

(2) Pale ambapo Kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kinapingana na mawazo ya Bodi ya Zabuni juu ya mapendekezo yake chini ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, Kitengo cha manunuzi na uuzaji mali kinaweza kuomba ushauri huru kutoka Mamlaka.

(3) Mbali ya kuomba ushauri kutoka Mamlaka chini kifungu kidogo (1) na (2) ya kifungu hiki, Kitengo cha manunuzi na uuzaji mali kitaeleza kwa maandishi sababu za kutokubaliana huko.

Kazi za Idara husika.

35.-(1) Idara husika ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali itafanyakazi zifuatazo-

(a) kushirikiana na kusaidiana na Kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kupitia taratibu za manunuzi au uuzaji mali za serikali kufikia kiwango cha kusaini mkataba;

(b) kutayarisha taratibu za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali na kuziwasilisha katika Kitengo cha Manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

(c) kupendekeza vitu halisi vinavyotarajiwa kuwa ni masharti ya zabuni kwa Kitengo cha Manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

(d) kupendekeza sifa za kiufundi kwa kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali itakapohitajika;

(e) kuingiza vitu muhimu katika tathmini ya zabuni kama zilivyopokewa na Kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali.

(f) kutayarisha malipo kwa wazabuni;

(g) kuwasilisha taarifa yoyote ya kutokufuata vigezo na masharti yaliowekwa katika mkataba kwa kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

(h) kuwasilisha taarifa zozote za ndani za mkataba unaotakiwa kufanyiwa marekebisho kwa hatua;

(i) kuweka na kuhifadhi taarifa za utekelezaji wa mikataba; na

(j) kutaraisha taarifa yoyote inayotakiwa kuwasilishwa katika Kitengo cha Manunuzi na Uuzaji wa mali za serikali, Kamati au Afisa Masuuli.

(2) Idara husika inatakiwa kutayarisha mpango wa manunuzi kulingana na bajeti iliyopishwa, ambayo itwasilishwa katika kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kwa kuchukuliwa hatua pale itakapohitajika.

Uwezo wa Idara husika.

36. Katika kufanya kazi zake, idara husika itakuwa-

(a) inatayarisha vigezo vitakavyotumika katika manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

(b) itapendekeza vigezo vinavyohitajika kwa Kitengo cha Manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

(c) itaangalia matokeo ya makadirio;

(d) kubadilisha agizo kwa mujibu wa vigezo na masharti ya mkataba; na

(e) kuthibitisha hati za malipo ya wazabuni.

Kutofautiana baina ya Kitengo cha manunuzi na Idara husika.

37. Pale ambapo Kitengo cha manunuzi na Uuzaji wa mali za serikali kitatofautiana na Idara husika kuhusiana na maamuzi yeyote yanayotokana na utumiaji au kutafsiri njia ya manunuzi, utaratibu au utumiaji, wahusika wanaweza kupeleka sababu za kutofautiana kama maelezo kwa Bodi ya Zabuni kwa ajili ya kutolewa maamuzi ya mwisho.

Kamati ya Tathmini.

38.-(1) Tathmini zote za zabuni lazima zifanywe na Kamati ya Tathmini, ambayo itatoa taarifa kwa Kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali.

(2) Wajumbe wa Kamati ya tathmini watapendekezwa na Kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kwa mujibu wa Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii, pamoja na kuthibitishwa na Bodi ya Zabuni.

(3) Idadi za wajumbe wa Kamati ya Tathmini itategemea thamani na ugumu wa kazi yenyewe, lakini wasiwe chini ya wajumbe watatu.

(4) Wajumbe wanatakiwa wawe katika kiwango cha juu na uzowefu, kulingana na uzito wa kazi ya manunuzi inatayotakiwa kufanywa.

(5) Wajumbe wa kamati ya tathmini wanaweza kuteuliwa kutoka nje ya taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali, pale itakapotokea kuwa ujuzi na uzoefu katika taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali haupatikani au itakapotekea kuwa wajumbe hawawezi kufanyakazi au wana mgongano wa maslahi.

(6) Wajumbe wote wa kamati ya tathmini wasaini hati ya kiapo iliowekwa ndani ya kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii, kuthibitisha kuwa hawana mgongano wa maslahi juu ya masharti ya manunuzi.

(7) Vikao vya kamati ya tathmini, kazi za kamati ya tathmin na utaratibu wa kufanya tathmini utatekelezwa kwa mujibu wa kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii.

Uhuru wa kufanya kazi.

39. Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, Afisa Masuuli, Bodi ya zabuni, kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali, idara husika na kamati ya tathmini zitafanyakazi zake bila ya kuingiliwa.

Kukasimu mamlaka kwa Afisa Masuuli.

40. Afisa Masuuli anaweza-

(a) kuchaguwa baadhi ya kazi za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali za Afisa Masuuli, Bodi ya Zabuni au Kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kwa-

(i) ugawaji wa taasisi za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali;

(ii) mfanyakazi wa taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali, na

(b) kupunguza baadhi ya kazi za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali kwa Bodi ya Zabuni, Kitengo cha manunuzi na uuzaji wa mali za serikali au idara husika kwa, taasisi nyengine ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali au kwa mujibu wa vigezo na masharti vilivyowekwa ndani ya kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii.

Kuthibitisha kutumia njia mbadala.

41.-(1) Taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali ambayo haiwezi kufuata utaratibu wa Sheria hii uliowekwa kwa manunuzi au uuzaji wa mali serikali, inaruhusiwa kuomba kwa Mamlaka kutumia njia utaratibu mwengine.

(2) Mamlaka itaruhusu kutumika kwa utaratibu mwengine wa manunuzi-

(a) pale ambapo mahitaji maalumu yamefanya isiwezekane, haitekelezeki au haitosaidia ikiwa itatumika Sheria hii;

(b) wakati ambapo hali ya soko au tabia hairuhusu utumiaji sahihi wa Sheria hii; na

(c) kwa kazi maalumu au masharti maalum ambayo yanasimamiwa au kuongozwa kwa kushirikiana na viwango au uzoefu wa kikamataifa.

(3) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Mamlaka inaweza kwa juhudi zake kuruhusu njia nyengine kwa taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali ambayo haikuweza kufuata taratibu za manunuzi na uuzaji wa mali kama zinavyotakiwa na Sheria hii.

(4) Mamlaka itathibitisha njia nyengine pale ambapo taasisi ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali-

(a) inafanya kazi sehemu maalum au taaluma ambayo inahitaji taratibu nyengine au kanuni nyengine;

(b) inahadhi ya kutumia njia nyengine au kanuni nyengine;

(c) inatakiwa kutumia njia nyengine ili iwe imefuata masharti ya kimataifa au makubaliano mengine, au

(d) ina sababu za msingi ambazo zinapelekea matumizi ya njia nyengine.

(5) Ombi la kuthibitisha lazima lifanywe kwa kutumia taratibu zilizowekwa katika kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii.

Kumbukumbu za taasisi za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali.

42.-(1) Taasisi za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali zitatunza na kuhifadhi kumbukumbu zinazohusiana na manunuzi ya taasisi kwa kipindi cha miaka saba kuanzia tarehe ambayo maamuzi ya kusitisha manunuzi au uuzaji yalifanywa, au tarehe ya kukamilika kwa mkataba, lolote litakalokuja baadae, isipokuwa pale mkataba unaendelea au unalalamikiwa, ambapo, kumbukumbu zake zitaongezwa

mwaka mmoja baada ya kukamilika au kutatuliwa kwa mgogoro, lolote litakalotangulia.

(2) Kumbukumbu zinazotakiwa kuangaliwa na taasisi za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali chini ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, zijumuishe muhtasari wa taarifa za taratibu za manunuzi zilizotumika katika kila mkataba, ambazo zitaonyesha-

(a) ufafanuzi wa malengo ya manunuzi yaliofanywa;

(b) orodha ya wazabuni walioshiriki;

(c) bei zilizotolewa;

(d) vigezo vilivyotumika kufanya tathmini;

(e) muhtasari wa tathmini iliyofanywa na ulinganishi wa zabuni, ikijumuisha sababu za kukataliwa kila zabuni;

(f) pale inapowezekana, muhtasari wa maelezo ya hatua za mapitio ya malalamiko yaliyofanywa pamoja na maamuzi yaliyochukuliwa;

(g) maelezo ya sababu za kusitisha mchakato wa manunuzi; na

(h) taarifa nyengine zozote kama zitakavyoelezwa na kanuni.

(3) Taarifa za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali zitakuwa wazi kwa ajili ya kukaguliwa na Mamlaka na mamlaka zinazofaa ndani ya muda wa kazi.

Vyombo vya ulinzi na usalama wa taifa.

43.-(1) Kwa kuondowa shaka, vyombo vya ulinzi na usalama vitafuata Sheria hii kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) na (3) vya kifungu hiki.

(2) Vyombo vya ulinzi na usalama vitafanya manunuzi yao na uuzaji wa mali za serikali kwa kuzingatia hesabu mbili, ikijumuisha manunuzi ya vitu yatakayokuwa na ushindani wa wazi na manunuzi yatakayofanywa bila ya ushindani au njia ya uuzaji peke yake.

(3) Vyombo vya ulinzi na usalama vitakubaliana na Mamlaka kwa kila mwaka juu ya bidhaa ambazo zitanunuliwa bila ya ushindani kuingizwa katika orodha za zabuni zilizokuwa sio za ushindani, ambapo utaratibu wa manunuzi yatakayofanywa bila ushindani umeelezwa katika sehemu nne, utatumika kwa kila aina ya bidhaa zilizotajwa katika orodha za zabuni zilizokuwa sio za ushindani.

(4) Orodha ya zabuni zitakazofanywa bila ya ushindani zitafanywa kwa mujibu wa ukaguzi utakaobainisha na kabla ya kupelekwa Baraza la Wawakilishi katika mkutano wa mwaka wa kupitia tathmini ya taarifa za utekelezaji.

(5) Vyombo vya ulinzi na usalama vitateua Bodi ya Zabuni itakayoshughulikia manunuzi na uuzaji wa bidhaa zao zitakazobainishwa.

(6) Wajumbe wa Bodi ya Zabuni ya vyombo vya ulinzi na usalama watateuliwa na Maafisa Masuuli wanaohusika na kuthibitishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

SEHEMU YA NNE
MISINGI YA MANUNUZI NA UUZAJI WA MALI ZA SERIKALI

Utekelezaji wa kanuni za msingi.

44. Manunuzi na uuzaji wa mali za serikali unatakiwa kufanywa kwa mujibu wa misingi ifuatayo-

(a) kutokuwa na ubaguzi;

(b) kwa uwazi, uwajibikaji na bila ya upendeleo;

(c) kuwepo na ushindani na kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana;

(d) kuwepo na siri;

(e) kuzingatia uchumi na uwajibikaji; na

(f) kuimarisha uadilifu na uaminifu.

Ushindani wa wazi wa zabuni.

45. Taasisi za manunuzi na uuzaji wa mali za serikali zinatakiwa kutumia ushindani wa wazi wa zabuni kama njia ya manunuzi na uuzaji wa mali za serikali.

Mshindi wa zabuni.

46. Mkataba utatolewa kwa mshindi wa zabuni aliyefanyiwa tathmini na kuonekana kushinda kulingana na utaratibu na vigezo vilivyowekwa katika nyaraka za zabuni.

Upatikanaji wa taarifa.

47. Nakala zote za fomu zilizowekwa katika Sheria hii, nyaraka za zabuni na maamuzi ya Mamlaka yatawekwa wazi kwa wananchi kuweza kuyaona.

SEHEMU YA TANO
KANUNI ZA UNUNIZI NA UUZAJI MALI

Kutumika kwa kanuni za ununuzi na uuzaji mali.

48. Miamala yote ya ununuzi na uuzaji mali za umma itafanywa kwa mujibu wa kanuni zilizoelezwa katika sehemu hii ya Sheria hii, pamoja na Kanuni na miongozo itakayotolewa chini ya Sheria hii.

Mawasiliano.

49.-(1) Mawasiliano yote baina ya taasisi ya ununuzi na uuzaji mali na mzabuni au mtoa huduma itakuwa kwa maandishi na mawasiliano ya aina nyengine itachukuliwa na kuthibitishwa kwa maandishi.

(2) Lugha ya kiingereza na kiswahili ndiyo itakayotumika katika mawasiliano isipokuwa pale itakavyoelezwa vyenginevyo na Mamlaka.

(3) Njia ya mawasiliano itaainishwa katika nyaraka za maombi ya zabuni.

Mpango wa ununuzi na uuzaji mali.

50.-(1) Kwa mujibu wa maandalizi ya taratibu za bajeti iliyotolewa na Waziri, taasisi ya ununuzi na uuzaji mali, kwa kila mwaka wa fedha katika tarehe itakayoelezwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali, itaandaa na kuwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na Mamlaka mpango wake wa mwaka wa ununuzi na uuzaji kwa mwaka unaofuata.

(2) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itapanga mpango wake wa ununuzi na uuzaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia-

(a) kulingana na mahitaji yake kwa namna inavyowezekana, baina yake na taasisi nyengine ya ununuzi na uuzaji mali, ili kupata thamani halisi ya fedha na kupunguza gharama za matumizi;

(b) kutumia mfumo wa mikataba kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kupata kazi, huduma au usambazaji wa bidhaa zinzohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda;

(c) kutotenganisha ununuzi au uuzaji kwa lengo la kutokutumia utaratibu wa ununuzi na uuzaji wa mali;

(d) kulinganisha bajeti ya ununuzi na mipango ya uuzaji mali; na

(e) kulinganisha uuzaji wa mali zote zilizoainishwa na ambazo hazikuainishwa katika daftari la kumbukumbu za mali pamoja na bajeti ya mapato na matumizi.

(3) Mamlaka itatoa miongozo kuhusiana na mfumo wa mpango wa ununuzi na uuzaji utakaoandaliwa chini ya kifungu hiki.

(4) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali kila baada ya miezi mitatu na kwa namna yoyote itakavyojitokeza, itafanya mapitio na kuboresha mpango wa ununuzi na uuzaji mali.

(5) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itamjuulisha Mlipaji Mkuu wa Serikali na Mamlaka mabadiliko yoyote itakayoyafanya katika mpango wake wa ununuzi na uuzaji mali na itawasilisha mpango ulioboreshwa na kuidhinishwa kwa Mamlaka.

(6) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itaweka katika ubao wa taarifa, mpango wake ulioboreshwa na kuidhinishwa au kwa kutumia utaratibu mwengine wowote utakaoelekezwa, si chini ya siku ishirini za kazi.

(7) Ununuzi hautofanyika kinyume na mpango wa ununuzi na uuzaji mali isipokuwa kwa hali ya dharura.

Mwanzo wa hatua za ununuzi na idhini ya fedha.

51.-(1) Mahitaji yote ya ununuzi lazima yafanywe kwa maandishi kabla ya kuanza taratibu za ununuzi au uuzaji wa mali.

(2) Ununuzi au uuzaji wa mali utaanzishwa au kuendelea baada ya kuidhinishwa fedha zote kwa kiwango chote kwa muda wote au kuwepo uwezo wa kupatikana fedha wakati wa kuanza mkataba.

(3) Mahitaji yote ya ununuzi au uuzaji wa mali lazima yaidhinishwe na Afisa Masuuli kabla ya kuanza hatua za ununuzi au uuzaji mali.

Mfumo unaokubalika.

52.-(1) Kwa kuzingatia sera za kiuchumi na kijamii za serikali na makubaliano ya kimatiafa kwa serikali, kipaumbele kitatolewa kwa bidhaa zinazozalishwa ndani, wahandisi wa Zanzibar, wataalamu elekezi wa Zanzibar, kwa ajili ya kukuza maendeleo yao, kwa kuwapa nafasi ya kiushindani katika mikataba ya ununuzi inapotolewa pamoja na bidhaa za kigeni, wahandisi wa kigeni au wataalamu elekezi wa kigeni.

(2) Kukuza sekta maalumu ndani ya eneo maalumu, mikataba ya ununuzi maalumu au baadhi ya mikataba itapewa kipaumbele kwa mpango wa upendeleo maalum.

(3) Mpango wa upendeleo maalum utatumika-

(a) kuhusiana na bidhaa, kazi na huduma za ushauri na zisizo za ushauri endapo utaratibu wa zabuni za ndani au zabuni za kimataifa umetumika, ukiwa na masharti maalum yamewekwa, mfumo wa upendeleo utazingatiwa wakati wa hatua ya kulinganisha na upembuzi wa gharama za fedha kwa mzabuni ambaye hakukidhi sifa za upendeleo; na

(b) kuhusiana na huduma za ushauri elekezi, kwa mfumo wa kuzingatia ubora na gharama nafuu na kwa kuzingatia gharama za chini, pale ambapo maombi yametakiwa kwa wataalam wa ndani na kimataifa, hata kama vigezo maalum vimeongezwa kwa zabuni za kimataifa, wakati wa hatua ya kulinganisha na upembuzi wa gharama za fedha.

(4) Vigezo maalum vilivyotajwa katika kifungu kidogo cha (1), itakuwa-

(a) kwa kuzingatia gharama, itaongezwa katika gharama za mzabuni ambaye hakukidhi sifa za upendeleo au mzabuni wa kimataifa aliyekubalika kutokana na mapendelekezo yake;

(b) kuhusiana na bidhaa iliyotengenezwa ndani, itahusika na asilimia ya kazi, rasilimali na vitu vyengine vya bidhaa ambavyo asili yake ni Zanzibar; na

(c) kuhusiana na kazi au huduma-

(i) kulingana na asilimia ya mtaji wa hisa ya mjenzi au mtaalam elekezi pale ambapo mtaalam elekezi ni kampuni inayomilikiwa na serikali au Mazanzibari; au

(ii) itazingatia gharama na kuongezwa katika gharama za mzabuni ambaye hakukidhi sifa zinazohitajika au gharama za mzabuni wa kimataifa, ikiwa mtaalam elekezi ni Mzanzibari.

(5) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali italazimika, pale ambapo inanunua bidhaa, kazi ya ujenzi au huduma chini ya kifungu hiki, kutoa upendeleo kiwango cha chini-

(a) cha asilimia kamsini, kwa bidhaa husika; na

(b) cha asilimia kumi kwa kazi ya ujenzi au huduma.

(6) Ubora wa bidhaa utakaokubalika kwa bidhaa za ndani, chini ya kifungu kidogo cha (2)(b) cha kifungu hiki, endapo-

(a) wafanyakazi au thamani ya bidhaa imeongezeka kwa zaidi ya asilimia thelathini ya kazi iliyofanywa au bidhaa; na

(b) vifaa vya uzalishaji ambavyo bidhaa zimetengenezwa, zimeandaliwa au kukamilishwa Zanzibar na anajishughulisha katika utengenezaji, uandaaji au ukamilishaji wa bidhaa wakati wa kuwasilisha zabuni.

(7) Mkandarasi na mshauri elekezi mwenye sifa za kupata upendeleo kama Mkandarasi au mshauri elekezi wa Mzanizbar chini ya kifungu kidogo (2)(c) endapo-

(a) mkandarasi au mshauri elekezi amesajiliwa Zanzibar;

(b) mkandarasi au mshauri elekezi ikiwa ni mtu binafsi, ni Mzanzibari;

(c) mkandarasi au mshauri elekezi ikiwa ni kampuni imesajiliwa Zanzibar, zaidi ya asilimia hamsini ya mtaji wa hisa wa kampuni ya kandarasi au ushauri elekezi inamilikiwa na Mzanzibari; na

(d) mkandarasi au mshauri elekezi ni taasisi, zaidi ya asilimia hamsini ya mtaji wake unamilikiwa na Serikali au taasisi ya ununuzi na uuzaji mali.

(8) Mkandarasi au mshauri elekezi aliyetimiza sifa hizo chini ya kifungu kidogo cha (5)(d) cha kifungu hiki, italazimika-

(a) kujitegemea kisheria na kifedha;

(b) kuanzishwa kibiashara; na

(c) imeidhinishwa na mamlaka yenye uwezo au taasisi ya kitaalam kufanyakazi kama mkandarasi au kutoa huduma za ushauri elekezi.

(9) Taasisi ya ununuzi na uuzaji wa mali italazimika, pale ambapo itaomba kazi ya ujenzi au huduma kwa pamoja au kwa mashirikiano baina mkandarasi Mzanzibari na mkandarasi wa kimataifa au baina mshauri lekezi wa Zanzibar na mshauri wa kimataifa, kuweka upendeleo kwa asimia nne kwa kazi au huduma hiyo.

(10) Kampuni ya pamoja au ushirika baina ya mkandarasi Mzanzibari na mkandarasi wa kimataifa au baina ya mshauri elekezi Mzanzibari na Mshauri elekezi wa kimataifa, itakuwa na sifa za kupata upendeleo pale ambapo-

(a) ushirika huo umesajiliwa Zanzibar;

(b) mkandarasi Mzanzibari au mshauri elekezi Mzanzibari ni ushirika wenye sifa ya kupata upendeleo chini ya kifungu kidogo cha (5); au

(c) mkandarasi Mzanzibari au mshauri elekezi Mzanzibari amethibitisha kupata faida zaidi ya asilimia hamsini katika ushirika huo kama alivyoainisha katika kipengele cha faida ya pamoja katika makubaliano yao.

Mpango wa uhifadhi.

53.-(1) Mamlaka kwa kushirikiana na mamlaka husika na wadau wanaohusika, itaainisha aina za mikataba ya ununuzi kuwa ni mfumo unaokubalika na itaainisha sakta mahususi ndani ya eneo litakaloainishwa kuruhusiwa kushiriki katika mpango huo.

(2) Mkataba wa ununuzi wa mali za umma itaandaliwa kwa kuzingatia mpango uliokubalika kwa ajili ya-

(a) kuendeleza kutumika kwa utaalamu na rasilimali za ndani;

(b) kuendeleza ushirikishaji wa jamii na jumuiya za ndani; au

(c) kutumia teknolojia mahususi.

(3) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali ambayo inakusudia kufanya ununuzi chini ya mpango unaokubalika italazimika-

(a) kuomba kwa Mamlaka ruhusa ya kutumia njia mbadala na nyaraka na katika kutumia njia hiyo itaainisha mfumo wa mkataba, viwango mbalimbali na utaratibu wa makubaliano utakaojumuishwa katika nyaraka za zabuni; na

(b) kushughulika na watoa huduma wenye sifa kushiriki katika mpango unaokubalika kwa mujibu wa masharti ya kifungu hiki.

(4) Utaratibu na nyaraka za ununuzi pamoja na aina ya mkataba, viwango na hatua nyengine za makubaliano zitakazotumiwa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, itakuwa kwa mujibu wa kanuni za ununuzi zilizoelezwa chini ya Sheria hii.

Maelezo ya mahitaji.

54.-(1) Maelezo ya mahitaji yanaweza kuwa katika mfumo utakaojumuisha-

(a) aina ya kazi;

(b) hadidu rejea;

(c) kiwango cha kazi;

(d) michoro;

(e) gharama za vifaa; au

(f) kitu kinacholingana na vitu vilivyoainishwa katika kifungu kidogo hiki, kadri itakavyohitajika.

(2) Maelezo ya mahitaji yataeleza kwa uhalisi na ukamilifu wa mambo yote ya kitu kinachonununliwa au kuuzwa na hatua zinazohusika ili kutoa ushindani ulio sawa.

Viwango vinavyokubalika.

55. Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itatumia wakati wote viwango vinavyokubalika katika fani husika na iliyokubaliwa katika jumuiya na fani za kimataifa na taasisi za kimataifa.

56.-(1) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itatumia nyaraka zenye viwango zilizoidhinishwa na Mamlaka kama ndio njia bora ya uandaaji wa nyaraka kwa kila muamala wa ununuzi au mahitaji ya uuzaji. Viwango vya nyaraka za zabuni.

(2) Nyaraka zote za zabuni zitaainisha-

(a) taarifa zinazojitosheleza za vigezo na masharti ambayo yatatumika katika mkataba; na

(b) masharti ya jumla ya mkataba au maelezo ya jumla ya mkataba yatakayotumika.

(3) Masharti ya jumla ya mkataba hayatobadilishwa isipokuwa kupitia kwa masharti mahususi yatakayoingizwa katika nyaraka au mkataba.

(4) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali italazimika kupata ruhusa ya Mamlaka kabla ya kubadilisha masharti ya kataba zaidi ya masharti yaliyomo katika nyaraka zilizotolewa na Mamlaka.

57. Taratibu zote za kuchagua wazabuni watakaalikwa kushiriki zitaruhusu ushindani ulio sawa na wa haki na kuhakikisha unashirikisha ushindani wa hali ya juu. Uteuzi wa wazabuni.

58. Kipindi cha zabuni kitatosheleza kuruhusu wazabuni kuandaa na kuwasilisha zabuni zao na hautopunguzwa kwa madhumuni ya kuzuia ushindani. Muda wa zabuni.

59.-(1) Wakati wowote kabla ya kumalizika muda wa kuwasilisha zabuni, taasisi ya ununuzi na uuzaji mali inaweza bila ya maombi au kutokana na maombi ya ufafanuzi kutoka kwa mzabuni, kuweka sawa nyaraka za awali za zabuni kwa kutoa nyongeza ya nyaraka. Ufafanuzi wa nyaraka za awali za zabuni.

(2) Pale ambapo taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itaona kuwa ni muhimu, inaweza kuongeza tarehe ya kufunga zabuni ili kuruhusu wazabuni kuchukua na kuzingatia kikamilifu nyongeza ya nyaraka na kuandaa zabuni zao.

60. Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itaagiza wazabuni kuwasilisha kwa maandishi zabuni zilizofungwa kwa lakiri isipokuwa pale itakapoelezwa vyenginevyo na Sheria hii au Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii. Utaratibu wa zabuni.

61. Utaratibu wa kuwasilisha zabuni, aina, mambo yanayohusika na uataratibu wa upembuzi utakaofantwa na taasisi ya ununuzi na uuzaji, utaelezwa katika Knauni zitakazotungwa chini ya Sheria hii. Utaratibu wa kuwasilisha zabuni.

62. Mzabuni anaweza kuweka sawa au kuondoa zabuni yake muda wowote kabla ya kipindi cha mwisho kilichowekwa cha kuwasilisha zabuni, kwa utaratibu kama utakavyoelezwa katika Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii. Kusawazisha na kuakhirisha zabuni.

63. Utaratibu wote wa zabuni utajumuisha utaratibu wa kupekea na kufungua zabuni kuliko rasmi. Kupokea na kufungua zabuni.

64. Taasisi ya ununiz na uuzaji mali itawaagiza wazabuni wote wanaoshiriki katika zabuni ya ununuzi au uuzaji mali, kutimiza vigezo vilivyoelezwa katika Sifa za msingi za wazabuni.

nyaraka za zabuni ambapo wakati wote watatakiwa kutimiza masharti ya sifa za msingi zifuatazo-

(a) kwamba mzabuni awe na uwezo wa kisheria kuingia katika mikataba;

(b) kwamba mzabuni asiwe-

(i) mtu aliyefilisika;

(ii) anayesimamiwa;

(iii) asiye na uwezo wa fedha; au

(iv) anayekusudiwa kufutwa;

(c) kwamba mzabuni amezuiliwa kufanya kazi;

(d) kwamba mzabuni anakesi mahakamani inayohusiana na lolote kati ya jambo lililotajwa katika aya ya (b).

Tathmini.

65.-(1) Utaratibu wa tathmini ya mzabuni utaamuliwa kutokana na aina, thamani na mambo mengine yanayohusiana na ununuzi au uuzaji mali.

(2) Nyaraka zote za awali za zabuni zitatakiwa kujazwa na kueleza kikamilifu utaratibu wa tathmini na vigezo ambavyo zitatumika.

(3) Hakuna vigezo vya tathmini mbali ya ule ulioelezwa katika nyaraka za zabuni hautozingatiwa.

(4) Taasisi ya ununuzi na uuzaji atahakikisha kwamba tathmini za zabuni unafanyika kwa haraka kwa mujibu wa taratibu wa Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii.

Mabadiliko ya taarifa za zabuni.

66. Hakutakuwa na mabadiliko au tofauti ya msingi ya zabuni, ikijumuisha mabadiliko ya gharama, baada ya tarehe na muda wa kufungwa kwa zabuni, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo katika Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii.

Ufafanuzi wa zabuni zilizopokelewa.

67. Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali inaweza kumuuliza mzabuni kutoa ufafanuzi juu ya zabuni yake ili kusaidia upembuzi na kutoa ufafanuzi wa ziada ambao unaweza kukamilisha upembuzi katika hatua ya mwisho ya zabuni, kwa mujibu wa utaratibu ulioelezwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Zuio la kufanya majadiliano.

68.-(1) Majadiliano juu ya gharama hayatofanyika baina ya taasisi ya ununuzi na uuzaji mali na mkandarasi, kuhusianana na mapendelezo ya mkandarasi, isipokuwa pale ambapo-

(a) utaratibu wa ushindani umetumika na mzabuni mmoja tu ndiye aliyejibu zabuni hiyo;

(b) utaratibu wa zanuni ya moja kwa moja umetumika; au

(c) zabuni ni kwa ajili ya kupata huduma ya ushauri elekezi.

(2) Majadiliano ya gharma chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, yatafanywa pale tu ambapo mzabuni bora amepatikana kutokana na upembuzi wa wazabuni au mapendekezo yamezidi makisio ya fedha za bajeti ya taasisi ya ununuzi na uuzaji mali.

(3) Kwa ajili ya majadiliano chini ya kifungu hiki, taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itachunguza kwanini gharama zimeongozeka bajeti ya taasisi ya ununuzi na uuzaji mali, na inaweza-

(a) kufuta utaratibu wa hatua za ununuzi na maombi mapya; au

(b) kujadiliana juu ya mzabuni aliyekidhi vigezo za zabuni kwa ajili kupata punguzo la viwango vya manunuzi.

Kurejeshwa kwa zabuni.

69.-(1) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali inaweza kukataa zabuni zote au zabuni yoyote wakati wowotw kabla ya kuidhinisha mkataba.

(2) Kukataliwa kwa wazabuni au mapendekezo ya wazabuni inaweza kufanyika endapo-

(a) kutakuwa na hatari katika ushindani;

(b) zabuni au mapendekezo hayalingani na nyaraka za zabuni au maombi ya mapendekezo na hadidu rejea;

(c) taarifa za kiuchumi au kitaalam za mradi zimebadilishwa; au

(d) wazabuni au mapendekezo zinajumuisha gharama kwa kiwango cha juu cha msingi kuliko makadirio ya fedha.

(3) Kukosokana kwa ushindani kutaamuliwa kwa misingi ya idadi ya wazabuni au watu maliowasilisha mapendekezo ya zabuni.

Mkataba.

70.-(1) Kwa madhumuni ya Sheria hii, maamuzi ya kukubaliwa zabuni sio mkataba.

(2) Kukubaliwa kwa zabuni hakutoidhinishwa na taasisi ya ununuzi na uuzaji mali, mpaka-

(a) muda ulioelezwa katika Kanuni chini ya Sheria hii umemalizika; na

(b) fedha yote iliyotengwa imeshapangwa kwa kipindi chote kinachohitajika.

(3) Kukubaliwa kutaidhinishwa kwa mkataba wa maandishi utakaosainiwa na pande zote, mtoa huduma na taasisi ya ununuzi na uuzaji mali baada ya masharti yaliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, yametimizwa kikamilifu.

(4) Uamuzi wa kukubaliwa tenda utatumwa kwa utaratibu kama ulivyoelezwa katika Kanuni ndani ya kipindi kilichoelezwa katika aya ya (a) ya kifungu kidogo cha cha (2) cha kifungu hiki.

(5) Kanuni zitaeleza aina za mikataba.

Mabadiliko ya mazingira ya zabuni.

71. Mabadiliko yoyote katika mazingira yoyote ya mzabuni wakati wa hatua za ununuzi au uuzaji mali ambayo yanaweza kuathiri uwezo wa mzabuni wa kutekeleza mkataba yatawasilishwa kwa Bodi ya zabuni na mzabuni husika.

Katazo kwa maofisa wa serikali.

72. Maafisa wa Serikali hawatoshiriki katika taratibu za zabuni isipokuwa pale ambapo kuna jambo mahususi limewasilishwa kwa Maofisa wa Serikali na taasisi ya ununuzi na uuzaji mali, kwa kuzingatia-

(a) tangazo la ndani na ushindani;

(b) gharama za mauzo sio zaidi ya thamani iliyoidhinishwa katika jambo husika;

(c) kukubaliana kwa mkuu wa kitengo cha manunuzi na uuzaji mali, Bodi ya zabuni na Afisa Masuuli; na

(d) nyaraka zote za kila zabuni iliyotolewa imehifadhiwa na taasisi ya ununuzi na uuzaji mali kwa ajili ya uchunguzi na kuwekwa kumbukumbu, Afisa Masuuli atawasilisha nakala ya nyaraka hizo kwa Mamlaka na ndani ya siku saba za kazi.

SEHEMU YA SITA
UTARATIBU WA UNUNUZI NA UUZAJI WA MALI

Kuchagua njia ya manunuzi.

73.-(1) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali italazimika-

(a) kwa ununuzi wa bidhaa, kazi za ujenzi na shughuli nyengine zisiokuwa za ushauri, kutumia utaratibu ulioelezwa katika kifungu cha 74 hadi 80 pamoja na masharti yaliyoelezwa katika Jadweli la tatu la Sheria hii; na

(b) kwa huduma za ushauri, kutumia masharti yaliyoelezwa katika kifungu cha 86 pamoja na masharti ya upatikanaji huduma za ushauri yaliyoelezwa katika jadweli la tatu la Sheria hii.

(2) Uteuzi wa utaratibu utakaotumika, utaidhinishwa na Bodi ya zabuni.

(3) Taasisi ya manunuzi na uuzaji mali italazimika kupata ruhusa ya Mamlaka kabla ya kutumia utaratibu mwengine mbali ya ule uliyoelezwa katika sehemu hii ya Sheria hii.

Ushindani wa zabuni za ndani.

74.-(1) Isipokuwa pale ilipoelezwa vyenginevyo katika Sheria hii au kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii, taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itatumia utaratibu wa wazi wa ushindani wa ndani wa zabuni.

(2) Ushindani wa zabuni za ndani ni utaratibu ya ununuzi au uuzaji, ambao watoa huduma wote wanaweza kushiriki kwa masharti yaliyo sawa baada ya kutangazwa kwa fursa ya ununuzi au uuzaji.

(3) Ushindani wa zabuni ya wazi wa ndani utatumika kwa ajili ya kupata ushindani wa hali ya juu kadri itakavyowezekana na ubora wa huduma kulingana na thamani yake.

(4) Hakuna kitakachomzuia mzabuni wa nje au wakimataifa kushiriki katika ushindani wa zabuni za ndani.

Ushindani wa zabuni za kimataifa.

75.-(1) Ushindani wa zabuni za kimataifa ni njia ya ununuzi au uuzaji ambayo watoa huduma wote wana haki ya kushiriki kwa masharti yaliyo sawa baada ya kutangazwa fursa ya ununuzi au uuzaji ambayo imekusudiwa hasa kupata wazabuni wa nje.

(2) Ushindani wa zabuni za kimataifa utatumika kupata ushindani wa hali ya juu kadri inavyowezekana na ubora wa huduma kulingana na thamani yake, hasa endapo watoa huduma wa ndani itakuwa ni vigumu kufikia kiwango hicho.

Ushindani kwa zabuni za ndani.

76.-(1) Ushindani wa zabuni za ndani ni utaratibu wa ununuzi au uuzaji ambao, wazabuni wamepatikana kwa mualiko wa moja kwa moja bila ya matangazo ya wazi.

(2) Ushindani wa zabuni za ndani unatumika kupata ushindani na ubora wa huduma kulingana na thamani yake, pale ambapo thamani au mazingira hayaruhusu kufuata utaratibu wa zabuni ya wazi.

Ushindani wa zabuni za kimataifa.

77.-(1) Ushindani wa zabuni za kimataifa ni utaratibu wa ununuzi au uuzaji ambao, wazabuni wanapatikana kwa kualikwa moja kwa moja bila ya matangazo na wazabuni wanaoalikwa inajumuisha zabanuni za kimataifa.

(2) Ushindani wa zabuni za kimataifa unatumika kupata ushaindani na ubora wa huduma kulingana na thamani yake kwa kadri itakavyowezekana ambapo thamani na mazingira hayahalalishi au kuruhusu utaratibu wa zabuni ya wazi na orodha ya wazabuni wanaofanyiwa mchujo inajumuisha wazabuni wa nje.

Utaratibu wa kutoa dondoo.

78.-(1) Utaratibu wa kutoa dondoo zilizopatikana kutokana na idadi ya watoa huduma.

(2) Utaratibu ya kutoa dondoo utatumika kupata ushindani na ubora wa huduma kulingana na thamani yake kwa kadri itakavyowezekana, ambapo thamani ya mali au mazingira maalum haya halalishi au kuruhusu uwazi au taratibu za zabuni zilizowekewa vikwazo.

(3) Utaratibu wa kutoa dondoo utatumika katika kazi na usambazaji.

Zabuni ya moja kwa moja.

79.-(1) Ununuzi au uuzaji wa moja kwa moja ni njia ambayo ununuzi au uuzaji hufanywa kutoka kwa chanzo kimoja pekee kwa ajili ya ununuzi au ambao mazingira maalum yanazuia kutumia njia ya ushindani.

(2) Ununuzi au uuzaji wa moja kwa moja utatumika kufanya ununuzi au uuzaji kwa wakati na kwa ufanisi endapo mazingira hayaruhusu ushindani.

Uuzaji wa thamani ndogo.

80.-(1) Ununuzi au uuzaji wa thamani ndogo ni njia ya ununuzi au uuzaji mdogo, ambao utatumika kwa ununuzi au uuzaji kwa mahitaji ya ununuzi au uuzaji wa vitu vyenye thamani ndogo sana.

(2) Ununuzi au uuzaji wa thamani ndogo utatumika kupata ununuzi na uuzaji unaozingatia ufanisi na wakati endapo thamani ya mali hairuhusu kutumia njia ya ushindani.

Njia za uuzaji mali za serikali.

81.-(1) Uuzaji wa mali za Serikali unaweza kufanywa kwa njia zifuatazo-

(a) kwa mnada;

(b) kwa zabuni;

(c) kwa makubaliano ya moja kwa moja;

(d) kuuzwa kwa Maafisa wa Serikali;

(e) kuharibu mali;

(f) ubadilishaji au ugawaji wa mali kwa aina nyengine za uuzaji;

(g) kuifanyia biashara

(h) kuihaulisha kwenda kwa mamlaka nyengine ya ununuzi na uuzaji; na

(i) kuitoa kama mchango.

(2) Endapo mali ya Serikali itachangiwa kwa chombo cha ununuzi au uuzaji itazingatia yafuatayo-

(a) hali ya usalama wa Taifa na masuala yanahuhusu maslahi ya umma;

(b) masula ya afya na usalama;

(c) masuala ya kisheria na haki za binaadamu;

(d) mazingatio ya mazingira; na

(e) mali isiyotumika na yenye thamani ndogo.

(3) Mchango utatumika endapo tu njia nyengine za uuzaji haziwezi kutumiwa na chombo cha ununuzi na uuzaji.

(4) Bila kujali kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, taasisi ya ununuzi na uuzaji haitouza mali zinazohitajika bila ya kuidhinishwa na Waziri.

(5) Masharti ya kifungu kidogo (1)(c) cha kifungu hiki, hayatotumika kwa uuzaji wa ardhi utakaofanywa na Waziri anayehusika na ardhi.

(6) Kwa ajili ya kuondoa shaka, masharti ya kifungu kidogo cha (2)(c) cha kifungu hiki, yatatumika kwa uuzaji wa ardhi iliyochini ya Waziri anayehusika na ardhi kwa niaba ya taasisi ya ununuzi na uuzaji mali.

(7) Katika kifungu hiki "mali inayohitajika" maana yake ni ardhi, jengo, meli, hisa na mali nyengine kama itakavyoainishwa, inayomilikiwa na Serikali iliyopo ndani au nje ya Zanzibar.

(8) Taratibu zilielezwa ndani ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, zitaelezwa ndani ya Kanuni zitazotungwa chini ya Sheria hii.

82. Maelezo ya ziada kuhusiana na taratibu za uteuzi wa watoa huduma zitaelezwa katika Kanuni. Uteuzi wa watoa huduma.

83.-(1) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itanunua huduma ya ushauri elekezi kwa kuchapisha taarifa kama inavyoonekana katika Jadweli la nne la Sheria hii, inayomtaka mtu kueleza dhamira ya kutoa huduma inayohitajika. Zabuni ya ushauri elekezi.

(2) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itaandaa, kutokana na maelezo iliyopokea kutokana na taarifa iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1), orodha ya mchujo ya Washauri elekezi ambao wanauwezo wa kufanya kazi inayohitajika.

(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo (1) cha kifungu hiki, taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itanunua huduma ya ushauri elekezi kwa kutumia orodha ya mchujo ya Washauri elekezi iliyotayarishwa-

(a) kutoka katika daftari la usajili wa watoa huduma la Mamlaka;

(b) kutokana na mapendekezo ya mamlaka yenye uwezo;

(c) kwa kutumia orodha ya watu wenye sifa ya taasisi ya ununuzi na uuzaji mali; au

(d) kwa kutumia orodha ya watu wenye sifa ya taasisi nyengine ya ununuzi na uuzaji mali.

(4) Taasisi ya ununuzi na uuzaji itanunua huduma za ushauri elekezi kwa kutumia masharti ya kifungu kidogo (3) cha kifungu hiki, endapo-

(a) huduma za ushauri elekezi zinazohitajika zinaweza kutolewa na idadi iliyochaguliwa ya Washauri elekezi tu;

(b) muda au gharama zinazohitajika kuchunguza na kutathimini idadi kubwa ya maelezo ya maslahi hailingani na thamani ya kazi inayokusudiwa kufanywa; au

(c) kuna hali ya dharura.

(5) Njia itakayotumika ya kuchagua washauri elekezi itaelezwa katika Kanuni zitakzotungwa chini ya Sheria hii, na itajumuisha-

(a) kuzingatia ubora na thamani;

(b) njia ya ubora;

(c) kiwango cha bajeti ya fedha;

(d) kiwango cha chini cha gharama; na

(e) sifa za mshauri elekezi.

(6) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali inaweza kufanya mashauriano na mshauri aliyeteuliwa lakini mashauriano hayo hayatofanywa na washauri tofauti kwa wakati mmoja.

(7) Bila ya kujali masharti ya kifungu hiki, endapo mazingra ya kipekee yamejitokeza kuzuia kutumika kwa njia ya ushindani na endapo masharti ya

kutumia njia ya zabuni iliyoelezwa katika jadweli la nne la Sheria hii yamejitosheleza, taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itateua mshauri elekezi mwenye sifa na uwezo wa kufanyakazi inayohitajika.

SEHEMU YA SABA
AINA ZA MKATABA

Kuchagua mkataba.

84.-(1) Taasisi ya Ununuzi na Uuzaji mali kuhusiana na kazi za ununuzi, itatumia aina za mkataba iliyoainishwa katika sehemu hii au ain azote kwa pamoja, kwa kutumia utaratibu ulioelezwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(2) Aina za mikataba zitakuwa ni-

(a) mkataba wa malipo ya gharama zote kwa pamoja;

(b) mkataba wa malipo ya awamu;

(c) mkataba wa kipimo cha kazi;

(d) mkataba wenye mfumo maalum;

(e) mkataba wa asilimia;

(f) mkataba wa kurejesha gharama;

(g) mkataba wa bei maalum;

(h) mkataba wa kudhibiti;

(i) mkataba wa malipo ya mafanikio.

Aina nyengine za mikataba.

85.-(1) Kwa ajili ya aina nyengine ya mkataba au utaratibu wa mkataba, mbali ya aina zilizotajwa katika kifungu cha 84, inajumuisha kukodi, kukodisha, kununua, kutoa leseni, kupangisha, kutoa haki miliki au utaratibu mwengine wowote inaohusisha kushajiisha sekta binafsi kutoa ufadhili, ujenzi, kufanyakazi na kufanya matengenezo ya miradi ya maendeleo au kukubali kufanya jambo, taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itaomba ushauri kutoka kwa Mamlaka juu ya utaratibu na nyaraka zinazoweza kutumika.

(2) Katika kifungu hiki, "utaratibu unaojumuisha kushajiisha sekta binafsi kutoa ufadhili, ujenzi, kufanyakazi na matengenezo ya miradi ya maendeleo au kukubali kufanya jambo" inajumuisha kutoa fedha kwa ajili ya kujenga, kutoa usafiri, kufanya yenyewe na mashirikiano baina ya serikali na sekta binafsi.

SEHEMU YA NANE
MAPITIO YA KIUTAWALA

Mapitio ya kiutawala.

86.-(1) Mzabuni anaweza kuomba kufanyiwa mapitio ya kiutawala kwa uachaji wowote au uvunjaji wa taasisi ya ununuzi na uuzaji kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, au Kanuni yoyote au miongozo iliyofanywa kwa mujibu wa Sheria hii au kwa mujibu wa masharti ya nyaraka za zabuni ukijumuisha uzoefu.

(2) Taasisi ya ununuzi na uuzaji itampa mzabuni ambaye anaomba kufanyiwa mapitio ya kiutawala-

(a) ufupisho wa hatua za tathmini;

(b) ulinganishaji wa zabuni, maombi au madondoo ukijumuisha vigezo vya tathmini vilivyotumika; na

(c) sababu za kukataa zinazohusiana na zabuni.

(3) Taarifa zilizotolewa na mzabuni chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, zitatumika kwa madhumuni ya mapitio ya kiutawala tu.

Mapitio ya Afisa Mahesabu.

87.-(1) Mzabuni ambaye hakuridhika na maamuzi ya taasisi ya ununuzi na uuzaji anaweza kufungua malalamiko kwa Afisa Masuuli wa taasisi ya ununuzi na uuzaji mali.

(2) Malalamiko ya mzabuni dhidi ya taasisi ya ununuzi na uuzaji mali yatakuwa-

(a) kwa maandishi na yatawasilishwa kwa Afisa Masuuli wa taasisi ya ununuzi na uuzaji mali pamoja na ada iliyopangwa, na nakla itapelekwa kwa Mamlaka; na

(b) yatafanywa ndani ya siku kumi za kazi kuanzia siku ambayo mzabuni amepata taarifa ya uamuzi huo au alitakiwa kujua, juu ya mambo yaliyopelekea kutokea malalamiko.

(3) Baada ya kupokea malalamiko pamoja na ada iliyopangwa, Afisa Masuuli atalazimika-

(a) kusimamisha maramoja mwenendo wa ununuzi; na

(b) kutoa uamuzi kwa maandishi, ndani ya siku kumi na tano za kazi, kwa kuainisha njia sahihi za kuchukuliwa, kama zitakuwepo, pamoja na kutoa sababu za uamuzi wake na kuwasilisha nakla ya uamuzi huo kwa Mamlaka.

(4) Endapo-

(a) Afisa Masuuli hatofanya uamuzi ndani kipindi kilichoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (3) (b) cha kifungu hiki; au

(b) mzabuni hakuridhika na uamuzi wa Afisa Masuuli, mzabuni anaweza kupeleka malalamika kwa Mamlaka ndani ya siku kumi za kazi kuanzia siku ya kutolewa uamuzi huo na Afisa Masuuli.

(5) Mkataba hautoweza kufungwa na Afisa Masuuli na mtoa huduma-

(a) wakati wa kipindi cha mapitio ya kiutawala; na

(b) kabla ya Mamlaka haijafanya maamuzi ya mwisho kuhusiana na lalamiko hilo lilowasilishwa kwa Mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha 88(3) cha Sheria hii.

Mapitio ya Mamlaka.

88.-(1) Baada ya kupokea lalamiko, Mamlaka bila ya kuchelewa itatoa taarifa juu ya lalamiko hilo kwa taasisi husika ya ununuzi na uuzaji mali, itazuia taasisi ya

ununuzi na uuzaji mali kufanya jambo jengine mpaka Mamlaka ilitolee maamuzi lalamiko hilo.

(2) Mamlaka, isipokuwa kama italifuta lalamiko-

(a) itazuia taasisi ya ununuzi na uuzaji mali kutochukua hatua nyengine; au

(b) itabatilisha maamuzi yote au sehemu ya jambo au maamuzi hayo ambayo si halali yaliyofanywa na taasisi ya ununuzi na uuzaji mali.

(3) Kabla ya kufanya maamuzi yoyote juu ya lalamiko, Mamlaka itawajuilisha wazabuni ambao wanauhusiano na lalamiko hilo na inaweza kuzingatia uwakilishwaji kutoka kwa wazabuni na kutoka kwenye taasisi ya ununuzi na uuzaji mali husika.

(4) Mamlaka itatoa maamuzi ndani ya siku ishirini na moja za kazi baada ya kupokea lalamiko, ikiainisha sababu za maamuzi yake na haki iliyotolewa, ikiwa ipo.

(5) Mzabuni ambaye hakuridhika na maamuzi yaliyotolewa na Mamlaka chini ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, anaweza kutafuta haki katika mahkama yenye uwezo kisheria.

SEHEMU YA TISA
MASHARTI MENGINEYO

Mipaka ya mikataba ya wajumbe wa chombo cha ununuzi na uuzaji.

89.-(1) Isipokuwa kama itaruhusiwa na Kanuni, taasisi ya ununuzi na uuzaji mali haitoingia mikataba na-

(a) mjumbe wa Bodi ya Wazabuni au kamati ya tathmini, mfanyakazi wa taasisi ya ununuzi na uuzaji mali au mjumbe wa Bodi ya Upimaji.

(b) mtu aliyeteuliwa kisiasa au kiutawala kusimamia taasisi ya ununuzi na uuzaji mali, ikimjumuisha Waziri, Afisa Masuuli au mjumbe wa taasisi ya ununuzi na uuzaji; na

(c) kampuni, endapo mtu aliyeainishwa katika aya ya (a) au (b) ya kifungu hiki ana nguvu ya udhibiti wa hisa.

(2) Mjumbe wa Bodi ya Zabuni, mjumbe wa kitengo cha Usimamizi wa ununuzi na uuzaji, mjumbe wa Bodi ya usimamizi wa taasisi ya ununuzi na uuzaji mali au mjumbe wa Bodi ya Upimaji ambaye ana mgongano wa maslahi ya ununuzi na uuzaji husika-

(a) hatoshiriki katika mwenendo mzima wa ununuzi na uuzaji; na

(b) hatoshiriki katika kufanya maamuzi yanayohusiana na mkataba wa ununuzi na uuzaji, baada ya kufungwa kwa mkataba wa ununuzi na uuzaji.

(3) "Mgongano wa Maslahi" ulioelezwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, kuhusiana na mtu ambaye ametajwa chini ya kifungu hiki, unajumuisha maslahi binafsi yanayohusiana au biashara inayohusiana na mtu huyo ambaye anajua au alipaswa kujua kama alitakiwa kuchukua jitihada sahihi kuhusiana na mazingira hayo.

(4) "Uhusiano" uliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, maana yake ni uhusiano wa kifamilia au mtoto wa kulea, wanandoa na wazee.

(5) Mtu ambaye ametajwa chini ya kifungu hiki atapaswa kueleza maslahi yake binafsi ambayo yanaweza kuingilia kati au yanayotegemewa kuingilia kati katika shughuli zake za kibiashara, pamoja na taaisis ya ununuzi na uuzaji mali.

(6) Mtu ambaye atakwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki itakua ametenda kosa la jinai na akipatikana na hatia atapaswa kulipa faini isiyozidi laki tano au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kinga ya kutokushtakiwa.

90. Hakuna hatua ya kisheria itakayochukuliwa dhidi ya mjumbe yoyote au mfanyakazi wa Mamlaka au wa taasisi ya ununuzi na uuzaji mali kwa kosa la kutenda au kuacha kutenda huko kumefanywa kwa nia njema katika kutekeleza majukumu yake aliyopewa chini ya Sheria hii.

Kanuni za utendaji.

91.-(1) Afisa wa Umma pamoja na mtaalam ambaye ameajiriwa kutoa huduma maalum atasaini Kanuni za Maadili ya Kiutendaji zilizoainishwa katika Jadweli la Nne la Sheria hii.

(2) Wafanyakazi, watoa huduma au wasambazaji watapaswa kusaini tamko la ridhaa za Kanuni za Maadili ya Kiutendaji zilizowekwa na Mamlaka muda baada ya muda.

Kusimamishwa kwa watoaji huduma.

92. Mamlaka inaweza, kwa upendekezaji wa taasisi ya ununuzi na uuzaji mali au baada ya uchunguzi wake, kumsimamisha mtoa huduma katika kushiriki juu ya hatua za ununuzi au uuzaji wowote wa umma kwa kipindi kitakachowekwa na Mamlaka, endapo-

(a) mtoa huduma amevunja Kanuni za Maadili za watoa huduma;

(b) Mtoa huduma ameondolewa katika hatua za manunuzi za wakala wa mataifa ambayo Zanzibar ni mwanachama;

(c) baada ya uchunguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu anayejitegemea aliyeteuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, mtoa huduma akaonekana kuwa ana kumbukumbu za kutotekeleza majukumu katika hali ya kuridhisha;

(d) mtoa huduma amepatikana na hatia kwa kosa la rushwa au vitendo vya udanganyifu chini ya Sheria hii;

(e) mtoa huduma ameshindwa kutekeleza majukumu yake yaliyoainishwa katika mkataba;

(f) mtoa huduma amesimamishwa na Bodi ya Kitaalam ya watoa huduma, kwa kosa la kutokuwa na madili ya kitaaluma;

(g) mtoa huduma ameonekana kushindwa kutekeleza majukumu yake yaliyoainishwa chini ya Sheria hii.

Makosa na adhabu.

93.-(1) Mtu atahesabika kuwa ametenda kosa akiwa-

(a) bila ya sababu ya msingi ameshindwa au amekataa kutoa habari, au kutoa nyaraka, kumbukumbu au taarifa inayotakiwa kwa mujibu wa aya (a) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 8;

(b) bila ya sababu ya msingi ameshindwa au amekataa kuitikia wito au amekataa kutoa vutabu vya hesabu, mipango au kutoa ushahidi kama inavyotakiwa na aya (b) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 8;

(c) kinyume na Sheria hii anamzuia au anaweka vikwazo ambavyo havistahiki kwa afisa yoyote au mfanyakazi wa Mamlaka au taasisi ya ununuzi au uuzaji mali katika kutekeleza kazi au uwezo wake aliopewa kwa mujibu wa Sheria hii;

(d) anashirikiana kufanya kosa la rushwa au vitendo vya udanganyifu, na akipatikana na hatia atapewa adhabu ya kulipa faini isiyozidi shilingi laki tano au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja.

(2) Afisa Masuuli, mjumbe wa Bodi ya Wazabuni, mjumbe wa Kamati ya tathmini, mfanyakazi wa Mamlaka au wa taasisi ya ununuzi na uuzaji mali ambaye-

(a) anashirikiana kufanya kosa la rushwa au vitendo vya udanganyifu wakati wa hatua za ununuzi au uuzaji;

(b) anajiingiza katika mambo ya rushwa au mambo ya udanganyifu wakati wa hatua za ununuzi au uuzaji, atakua ametenda kosa la jinai na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tano au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja.

(3) Afisa Masuuli ambaye anasaini mkataba kinyume na -

(a) masharti ya kifungu cha 26(2) cha Sheria hii, atakua ametenda kosa la jinai na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki mmoja au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja;

(b) masharti ya kifungu cha 26(5) cha Sheria hii, atakua ametenda kosa la jinai na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tano au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja na pia anaweza kuagizwa na mahkama kulipa kiwango kinachofanana au tofauti na bei baina ya bei iliyolipwa kwa usambazaji, huduma au kazi na bei ya soko.

(4) Endapo itathibitika kwamba mtoa huduma anajihusisha na vitendo vya udanganyifu katika mwenendo wowote wa ununuzi-

(a) mtoa huduma huyo ataondolewa na Bodi ya Zabuni katika mlolongo wa ununuzi;

(b) Bodi ya Zabuni itapendekeza kwa Mamlaka kumsimamisha mtoa huduma huyo.

(5) Endapo mtoa huduma atasimamishwa chini ya Sheria hii, na ikiwa kuna mkataba baina ya mtoa huduma huyo na taasisi ya ununuzi na uuzaji, taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itakuwa na hiari ya kuubatilisha mkataba au kuendelea nao.

(6) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (4) na (5) cha kifungu hiki, taasisi ya ununuzi na uuzaji mali inaweza kuomba shufaa yoyote ya kisheria dhidi ya mtoa huduma.

(7) Endapo taasisi ya ununuzi na uuzaji mali, baada ya uchunguzi wa kina, ikaridhika kwamba mzabuni aliyefanya maombi ya kupewa mkataba, anajihusisha na mambo ya rushwa au vitendo vya udanganyifu katika kushindana kwa ajili ya upataji wa mkataba uliyopo, taasisi ya ununuzi na uuzaji mali inaweza-

(a) kukataa maombi ya upataji wa mkataba; au

(b) kupendekeza kwa Mamlaka kwamba mzabuni asimamishwe kushiriki katika hatua yoyote ya ununuzi au uuzaji.

(8) Endapo itabainika baada ya uchunguzi maalum wa mahkama kwamba mzabuni amejihusisha na mambo ya rushwa au vitendo vya udanganyifu wakati wa hatua za ununuzi, katika kupata mkataba au katika utekelezaji wa mkataba, Mamlaka itamsimamisha mzabuni kutoshiriki katika hatua yoyote ya ununuzi au uuzaji.

Kanuni.

94.-(1) Kwa mapendekezo ya Mamlaka, Waziri atatunga Kanuni kwa utekelezaji bora wa madhumuni na majukumu ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri atatunga, kwa mapendekezo ya Mamlaka, na kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi, Kanuni za ununuzi na uuzaji kwa chombo cha ununuzi na uuzaji nje ya Zanzibar.

(3) Kanuni zilizotungwa chini ya kifungu hiki zinaweza kueleza mgongano wa vifungu vyovyote vya Kanuni au miongozo yoyote iliyotungwa chini ya Sheria hii.

Miongozo.

95. Kwa utekelezaji bora wa madhumuni na majukumu chini ya Sheria hii, Mamlaka itatoa miongozo na kuichapisha katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Masharti ya mpito.

96.-(1) Isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo chini ya Sheria hii, Sheria hii itakuwa kigezo juu ya sheria zote zinazoanzisha Bodi ya Zabuni au mambo yanayofanana, taasisi za ununuzi na uuzaji mali ndani ya miezi kumi na mbili baada ya Sheria hii kuanza kutumika, kufanya shughuli zao kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Hatua za manunuzi na uuzaji ambazo zimefanywa kabla ya kuanza kwa Sheria hii zitaendelea kufanya kazi na kukamilishwa chini ya Sheria hii.

Kufutwa na kubakiza.

97.-(1) Sheria ya Manunuzi ya Serikali na Uuzaji wa Mali za Serikali Nam. 2 ya 2005 inafutwa.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitu au mapatano yoyote ya kibiashara yaliyofanywa kwa mujibu masharti ya Sheria iliyofutwa, kabla ya Sheria hii kuanza kutumika, itachukuliwa kuwa kama zimefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

JADWELI LA KWANZA
KIAPO CHA TAMKO
[Chini ya kifungu cha 14(4)(a)]

Mimi, ……. naapa kwamba nitafuata kanuni za Mamlaka ya Ununuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali ukijumuisha misingi ya haki za kimaumbile, usawa, kanuni za maadili ya kiutendaji na uzoefu katika kutekeleza majukumu yangu kama mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Ununuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali.
Vilevile nathibitisha kwamba sina maslahi yoyote kupitia mimi mwenyewe au kupitia mtu mwengine katika kipengele kitakachopelekea kutokezea kwa mgongano wa kimaslahi au kusababisha kumpendelea mtu yoyote kwa kupitia mimi mwenyewe au mtu mwengine aliehusishwa katika orodha ya vipengele maalum.

Na vilevile, kwa muda wote, nitalinda siri kwa kiwango kinachotakiwa na kwa viwango cha kitaalam katika kutekeleza majukumu yangu kama mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi.

Imekubaliwa na kutolewa tamko na mimi katika…….....tarehe …….Mwezi……, 20……

Imesainiwa na ……..... mjumbe wa Bodi.

JADWELI LA PILI

MUUNDO WA BODI YA ZABUNI
[Chini ya kifungu cha 28(1)]

Bodi ya Zabuni itaundwa na wajumbe wafuatao-

(a) Mwenyekiti;

(b) Wakuu wa Idara; na

(c) Wajumbe watatu watakaoteuliwa na Afisa Masuuli mmoja miongoni mwao awe na taaluma ya sheria.

JADWELI LA TATU

MASHARTI YA KUTUMIA NJIA ZA UNUNUZI
[Chini ya kifungu cha 73(1)]

Zabuni ya wazi ya ndani.

1.-(1) Zabuni ya wazi ya ndani itakuwa wazi kwa wazabuni wote baada ya kutangazwa kwa Taarifa ya Zabuni angalau katika gazeti mmoja la kitaifa.

(2) Nyaraka za Zabuni zitatolewa kwa mzabuni anaetumainiwa kwa malipo, kwa harama ambazo zimekubaliwa na Bodi ya Zabuni inayohusika.

(3) Ufunguzi wa zabuni ya umma itaongozwa kwa mujibu wa utaratibu utakaoelezwa na Kanuni.

Zabuni ya wazi ya Kimataifa.

2.-(1) Zabuni ya wazi ya Kimataifa inaweza kutumika badala ya zabuni ya wazi ya ndani endapo ushindani hautofanyika vizuri bila mzabuni wa kigeni au endapo zabuni za kigeni zitaongeza thamani yake.

(2) Hakuna kitu ambacho kitazuia mzabuni wa ndani kushiriki katika zabuni za wazi za kimataifa.

(3) Hatua za ununuzi chini ya zabuni za wazi za kimataifa zitafuata hatua za ununuzi ambazo zitawekwa na Kanuni.

(4) Zabuni za wazi za kimataifa zitakuwa wazi kwa wazabuni wote kupitia matangazo ya umma ya taarifa ya zabuni kwa uenezaji kimataifa.

(5) Nyaraka za zabuni zinaweza kutolewa kwa wazabuni wanaotumainiwa kwa malipo, kwa harama ambazo zimekubaliwa na Bodi ya Zabuni lakini, katika mazingira ambayo yatasimamiwa na miongozo.

(6) Ufunguzi wa zabuni ya umma utafanyika kwa mujibu wa utaratibu zilizoelezwa na Kanuni.

Zabuni za ndani zisizokuwa za wazi.

3.-(1) Zabuni za ndani zisizokuwa za wazi zinaweza kutumika endapo-

(a) usambazaji, kazi au huduma ambazo zinapatikana tu kwa idadi maalum ya watoa huduma; au

(b) hakuna muda wa kutosha kwa utaratibu wa wazi wa zabuni katika hali ya dharura; au

(c) thamani inayokadiriwa ya ununuzi haizidi kiwango cha awali kilichoelezwa katika miongozo ya ununuzi iliyowekwa chini ya Sheria hii.

(2) Hatua za manunuzi kwa zabuni za ndani zisizokuwa za wazi zitafuata taratibu za manunuzi zilizoelezwa na Kanuni na kama zifuatazo-

(a) mialiko ya zabuni itatolewa kwa wazabuni wanaokubalika bila ya kutangaza katika ubao wa matangazo;

(b) uchaguaji wa wazabuni utakuwa kwa mujibu wa taratibu zilizoelezwa na Kanuni; na

(c) ufunguaji wa zabuni za umma utafanyika kwa mujibu wa taratibu zilizoelezwa na Kanuni.

Zabuni za kimataifai zisizokuwa za wazi.

4.-(1) Zabuni za kimataifai zisizokuwa za wazi zinaweza kutumika wakati wa kusambaza, kazi au huduma inayopatikana kutoka kwa idadi ya watoa huduma maalum na-

(a) hakuna muda wa kutosha kwa taratibu za zabuni za wazi katika hali ya dharura; au

(b) thamani inayokadiriwa ya manunuzi haitozidi kiwango cha awali kilichoelezwa katika miongozo ya manunuzi.

(2) Hatua za manunuzi kwa zabuni za kimataifai zisizokuwa za wazi hazitofuata taratibu zilizoelezwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii kama zifuatazo-

(c) mialiko ya zabuni itatolewa kwa wazabuni wanaokubalika bila ya kutangaza katika ubao wa matangazo;

(d) uchaguaji wa wazabuni utakuwa kwa mujibu wa taratibu zilizoelezwa na Kanuni; na

(e) ufunguaji wa zabuni za umma utafanyika kwa mujibu wa taratibu zilizoelezwa na Kanuni.

Uanishaji.

5.-(1) Uanishaji unaweza kutumika endapo-

(a) hakuna muda wa kutosha kwa taratibu za zabuni za wazi katika hali ya dharura; au

(b) endapo thamani inayokadiriwa ya manunuzi haitozidi kiwango cha awali kilichoelezwa katika miongozo ya manunuzi.

(2) Hatua chini ya dondoo za manunuzi zitakuwa kama ifuatavyo-

(a) nyaraka muhumi zitatolewa kwa wazabuni wanaokubalika bila ya kutanga katika ubao wa matanagzo;

(b) uchaguaji wa wazabuni utakuwa kwa mujibu wa taratibu zilizoelezwa na Kanuni iliyotungwa chini ya Sheria hii;

(c) chombo cha ununuzi na uuzaji utapata angalau zabuni tatu; na

(d) ufunguzi wa zabuni za ndani utafanywa kwa mujibu wa taratibu zilizoelezwa na Kanuni.

Manunuzi ya moja kwa moja.

6.-(1) Manunuzi ya moja kwa moja yanaweza kufanyika-

(a) endapo-

(i) kutakuwa hakuna muda wa kutosha kwa utaratibu mwengine katika hali ya dharura;

(ii) kazi, huduma au usambazaji unapatikana kutoka kwa mtoaji mmoja tu;

(iii) mkataba ulokuwepo unaweza kurefushwa kwa kazi za ziada, huduma au usambazaji unaofanana na ikawa hakuna faida itakayopatikana kwa ushindani wa ziada, ikiwa thamani ya mkataba ulirefushwa ni wa maana.

(iv) kazi za ziada, huduma au usambazaji unapaswa kulingana na kazi, huduma au usambazaji uliokuwepo na ikawa kuna faida itakayopatikana kwa ushindani wa ziada kutoka kwa msambazaji wa awali aliyotoa thamani ya mkataba wa ziada; au

(v) ni muhimu au inapendekezwa kununua kazi za ziada, huduma au usambazaji kutoka kwa msambazaji wa awali kwa ajili ya kuhakikisha uendelezaji wa kazi za awali, ikijumuisha uendelezaji wa njia za kifundi, utumiaji wa uzoefu alioupata au kuendeleza makosa ya kitaalam, ikiwa thamani ya mkataba wa ziada ni wa maana;

(b) mazingira yaliyoelezwa katika aya ndogo (1)(a)(iii), (iv) na (v), endapo thamani ya kazi, huduma au usambazaji haizidi asilimia kumi na tano ya thamani ya mkataba wa mwanzo au uliokuwepo na mkataba wa mwanzo au uliokuwepo umetolewa kupitia hatua za ushindani; na

(c) endapo manunuzi ya moja kwa moja yamefanywa zaidi ya mara moja katika mazingira yaliyoelezwa katika aya ndogo ya (1) (b), thamani ya kukusanya kidogo kidogo kwa kazi zote mpya, huduma au usambazaji usizidi asilimia ishirini na tano ya thamani ya mkataba wa mwanzo au uliokuwepo.

Ununuzi mdogo.

7.-(1) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali itatumia njia ya ununuzi mdogo kwa mahitaji ambayo hayakutegemewa amabayo makadirio ya thamani yake ni chini ya kiwango cha awali kilichoelezwa.

(2) Endapo taasisi ya ununuzi na uuzaji mali inajihusisha na manunuzi madogo-

(a) gharama ya awali au risiti inayothibitisha usambazaji wa vitu vilivyonunuliwa na thamani iliyolipwa itapatikana na kwa kusainiwa na afisa wa usambazaji wa manunuzi;

(b) itakuwa ni jukumu la kuhakikisha kwamba thamani ya fedha inapatikana kwa kiwango cha utekelezaji chini ya utaratibu wa manunuzi; na

(c) uhusiano wa angalau dondoo tatu utafanywa.

(3) Taasisi ya ununuzi na uuzaji mali haitotumia ununuzi mdogo-

(a) kuvunja manunuzi kwa ajili ya kuzuia kutumia njia sahihi za manunuzi; au

(b) kwa manunuzi ya kazi, huduma au usambazaji endapo itahitajika kipindi cha muda maalum ikiwa cha mfululizo au cha kujirejea rejea ambacho mfumo wa mkataba unahitaji.

Taarifa ya mualiko wa kuainisha dhamira ya kutoa huduma ya ushauri uelekezi.

8. Taarifa ya mualiko wa kuainisha dhamira ya kutoa huduma ya ushauri uelekezi itatakiwa-

(a) kujumuisha jina na anuani ya taasisi ya ununuzi na uuzaji mali na maelezo mafupi ya huduma inayotakiwa; na

(b) kuchapishwa katika gazeti kwa machapisho mapana na endapo itawezekana, kwa biashara husika au uchapishaji wa kitaalam.

JADWELI LA NNE

KANUNI ZA MAADILI YA KIUTENDAJI ZA KAZI
[Chini ya kifungu cha 91(1)]

Misingi ya maadili.

1.-(1) Wafanyakazi hawatotumia mamlaka au afisi zao kwa maslahi yao binafsi na watapaswa kutafuta njia za kukuza hadhi ya Serikali ya Zanzibar nyumbani na nje kwa-

(a) kulinda kiwango sahihi cha uadilifu kwa kazi zote za ndani na nje ya taasisi ambazo zimewaajiri;

(b) kukuza viwango vya juu vya uwezo vya kiutendaji;

(c) utumiaji mzuri wa mali ambazo zinahusiana na utowaji faida kubwa kwa Zanzibar; na

(d) kufuata elimu na kuwa na ari kwa-

(i) sheria za Zanzibar na kanuni;

(ii) matendo ya shughuli zinazokubalika katika soko la kibiashara; na

(iii) masharti ya kimkataba.

Mgongano wa maslahi.

2. Wafanyakazi watapaswa kutaja maslahi yao yoyote binafsi ambayo yanaweza kuyatumia kwa shughuli zao.

Usiri na usahihi wa habari.

3.-(1) Wafanyakazi wataheshimu usiri wa habari ambazo watazipata wakati wa utekelezaji wa shughuli zao na hawapaswi kutumia habari hizo kwa maslahi yao binafsi.

(2) Habari ambazo watazipata wafanyakazi wakati wa utekelezaji wa shughuli zao zitapaswa kuwa za kweli na za haki na hazikutungwa kwa lengo la kupotosha.

Ushindani.

4. Wafanyakazi watajiepusha na mipango ya shughuli ambazo zinaweza kuzuia ufanyakaji wa ushindani kwa haki.

Zawadi ya kikazi.

5. Wafanyakazi hawatopokea zawadi ya kikazi kutoka kwa wasambazaji wa Serikali wa sasa au watakaokuja isipokuwa zawadi hiyo iwe na thamani ndogo kama vile kalenda au kalamu.

Ukarimu.

6. Wafanyakazi watajiepusha kufanya kazi katika hali ya huruma ambayo inaweza kuonekana na watu wengine kwamba ni upendeleo katika kufanya maamuzi ya shughuli za kiserikali au ni matokeo ya huruma.

Kikwazo cha kutumia habari.

7. Mjumbe wa Mamlaka, mjumbe wa taasisi ya ununuzi na uuzaji mali au mtaalam aliyeajiriwa kwa ajili ya kutoa huduma maalum hatotumia habari alizozipata kupitia uhusiano wake na Mamlaka au wa taasisi ya ununuzi na uuzaji

kwa kipindi cha mwaka mmoja baada ya kuhama katika afisi hiyo au baada ya kusita kutoa huduma maalum.

Ufafanuzi.

8. Katika jadweli hili, "mfanyakazi" maana yake ni afisa wa umma na mtaalam.

MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya Mswada huu ni kufuta Sheria ya Manunizi na Uuzaji Mali za Umma Nam. 9 ya 2005 na kutunga Sheria mpya inayoanzisha Mamlaka ya Manunuzi na Uuzaji Mali za Umma pamoja na mambo yanayohusiana na hayo. Mamlaka inayoanzishwa itakuwa ni chombo kinachojitegemea itakayokuwa na uwezo wa kushitaki na kushitakiwa na kuwa na mambo yote muhimu kama chombo kinachojitegemea.

Kazi za msingi za Mamlaka ni pamoja na-

(a) kuishauri serikali kuu, halmashauri za wilaya na taasisi nyengine za ununuzi na uuzaji mali za serikali katika masuala yote yanayohusiana na ununuzi na uuzaji mali za umma, sera, kanuni za msingi pamoja na mambo yanayokubalika;

(b) kusimamia na kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa mfumo wa ununuzi na uuzaji mali za umma kwa Zanzibar na kushauri juu ya mabadiliko yaliyobora zaidi;

(c) kuandaa, kuziendeleza na kutoa viwango vinavyokubalika kuhusiana na zabuni, nyaraka za zabuni, taratibu za fomu pamoja na nyaraka nyengine kwa taasisi za ununuzi na uuzaji mali za umma;

(d) kutoa miongozo mbalimbali inayohusiana na viwango vya ununuzi na uuzaji mali za umma vitakavyotumika na taasisi za serikali katika mambo ya ununiz na uuzaji mali za umma; na

(e) kazi nyengine nyingi kama zilivyoelezwa katika Mswada.

Mbali ya mambo hayo, Mamlaka itakuwa na uwezo wa kushughulikia malalamiko yatakayojitokeza katika miamala ya ununuzi na uuzaji wa mali za umma.

Mamlaka itakuwa chini ya uongozi na usimamizi wa Mkurugenzi Mtendaji ambaye atateuliwa na Rais. Mtu atafaa kuteuliwa katika nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji ikiwa ni Mzanzibari mwenye elimu ya angalau shahada ya kwanza katika fani ya ununuzi na usambazaji mali, usimamizi wa mali, uhandisi, fedha, uchumi, sheria au fani nyengine inayolingana na hizo kutoka katika Chuo kinachotambulika; na uzoefu wa kazi kwa kipindi kisichopungua miaka kumi na tano katika fani hiyo, na angalau miaka kumi akifanya kazi katika fani ya ununuzi au uongozi au utawala katika utumishi wa umma.

Mamlaka itakuwa chini ya usimamizi wa Bodi ya Wakurugenzi itakayoundwa na Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais na wajumbe wengine

kutoka katika fani mbalimbali serikalini na katika sekta binafsi zinazohusiana na mambo ya ununuzi, watakaoteuliwa na Waziri. Muundo wa Bodi unaopendekezwa utakuwa ni bora na kutoa michango iliyobora katika kusimamia kazi za Mamlaka kwa ujumla. Bodi inapendekezwa kuwa na wajumbe wataalam wa fani tofauti ikijumuisha sekta binafsi ili kwenda sambamba na dhana ya mashirikiano baina ya serikali na sekta binafsi (PPP).

Kazi za msingi za Bodi, pamoja na nyenginezo inajumuisha-

(a) kusimamia na kudhibiti uongozi katika kazi za Mamlaka;

(b) kusimamia utekelezaji wa masharti yanayohusiana na unuzi na uuzaji wa mali za umma;

(c) kuamua juu ya uteuzi na uajiri wa watumishi wa Mamlaka na kuwapangia kazi watumishi hao na kuweka vigezo na mashari ya kazi ikijumuisha kupandisha vyeo, kusimamisha kazi na hatua za kinidhamu;

(d) kuandaa mikakati, mipango na matarajio ya kazzi kwa kila idara ya Mamlaka; na

(e) kufanya kazi nyengine yoyote itakayopangiwa na sheria.

Imegundulika kwamba, Sheria iliyopo sasa ya manunuzi na uuzaji mali za umma inamapungufu mengi. Miongoni mwa mapungufu hayo ni pamoja na-

(a) masharti kuhusiana na manunuzi na uuzaji mali kwa serikali za mikoa;

(b) kuwepo kwa urasimu mkubwa katika taratibu za manunuzi na uuzaji wa mali za umma hasa katika uuzaji wa mali zilizochakaa;

(c) kukosekana kwa masharti kuhusiana na aina za viwango vya awali kwa aina mbalimbali za bidhaa, kazi na huduma za ushauri elekezi;

(d) kukosekana kwa masharti kuhusiana na muundo wa Bodi za Zabuni kwa mamlaka za Serikali za Mitaa na Halmashauri za Wilaya;

(e) Wakuu wa Idara za Serikali, mashirika na taasisi nyengine za Serikali kuwa Wenyeviti wa Bodi za Zabuni katika taasisi zao wakati huo huo wao ni maafisa masuuli katika taasisi hizo;

(f) Kuwepo kwa kiwango kidogo kwa miamala ya manunuzi;

(g) Kukosekana kwa chombo kinachojitegemea kusimamia miamala ya ununuzi na uuzaji mali za umma;

(h) Kukosekana kwa masharti yanayokubalika katika miamala ya ununuzi na uuzaji wa mali za umma; na

(i) Sheria kutoendana na sheria za manunuzi za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kutokana na mapungufu hayo, sheria mpya inayopendekezwa imezingatia kwa kiasi kikubwa maeneo yote yaliyotajwa hapo juu pamoja na kuzingatia mambo yafuatayo-

(a) Kutanua upeo wa matumizi ya sheria kwa serikali kuu na serikali za mitaa, taasisi zote za serikali na mashirika ya umma;

(b) Kanuni za msingi na utaratibu wa manunuzi na uuzaji mali za umma;

(c) Kuweka masharti kuhusiana kuanzisha mfumo wa usimamizi wa manunuzi na kushughulikia malalamiko yatakayojitokeza katika miamala ya manunuzi na uuzaji mali za umma;

(d) Kuanzisha na kuweka muundo wa taasisi za kushughulikia manunuzi na uuzaji mali za umma na kuweka uwazi katika miamala ya manunuzi na uuzaji mali za umma;

(e) Kuanzisha Bodi za Zabuni kwa kila idara ya Serikali, Shirika la umma, Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi, Kamati ya Tathimini, na mambo mengine yanayohusiana na hayo katika serikali kuu na serikali za mitaa ikijumuisha pia katika mashirika ya umma na taasisi za seriklai zinazojitegemea;

(f) Kuainisha aina maalum za mikata itaakayotumiwa na taasisi za umma pamoja na taratibu zitakazotumika sambamba na mikataba hiyo;

(g) Kutoa kipau mbele kwa kampuni za ndani (Zanzibar Companies);

(h) Ununuzi na uuzaji kwa njia ya mtandao;

(i) Kuweka utaratibu kwa ununuzi na uuzaji wa mali ghafi za serikali "fixed assets";

(j) Kuweka utaratibu wa wazi wa zabuni katika ununuzi na uuzaji mali za umma; na

(k) Mambo mengine yanayohusiana na masuala ya ununizi na uuzaji mali za umma.

Mswada huu umegawika katika sehemu Tisa, kama zinavyoelezwa kwa ufupi kama ifuatavyo-

Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi ambayo inajumuisha jina fupi na kuanza kutumika kwa sheria, kutumika kwa sheria na tafsiri ya baadhi ya maneno muhimu yaliyotumika ndani yake.

Sehemu ya Pili inahusu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uuzaji wa Mali za Umma, ambapo pamoja na mambo mengine inajumuisha malengo ya Mamlaka, kazi za Mamlaka, Uwezo wa Mamlaka, kuanzishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi, muundo wa Bodi, kazi za Bodi, uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji, sifa za Mkurugenzi Mtendaji, watumishi wengine wa Mamlaka na mambo mengine yanayohusiana na Bodi ya Wakurugenzi kwa ujumla.

Sehemu ya Tatu inahusu taasisi za ununuzi na uuzaji mali ambapo inajumuisha uwezo wa taasisi za ununuzi na uuzaji mali, Afisa Masuuli, Bodi ya Zabuni, kazi za Bodi ya Zabuni, uwezo wa Bodi ya Zabuni, kuanzishwa kwa Kitengo ch Ununuzi na Uuzaji, kazi za Kitengo, kazi za Idara zinazohusika, Kamati ya Tathmini, kukasimu madaraka kwa Afisa Masuuli, kukubalika kwa njia mbadala, kumbukumbu za taasisi za ununuzi na uuzaji mali na mambo mengineyo.

Sehemu ya Nne inahusu Kanuni za Msingi za Ununuzi na Uuzaji ambapo inajumuisha kutumika kwa kanuni za msingi, ushindani wa wazi wa zabuni, kuteuliwa kwa wazabuni bora na kuweka wazi taarifa za zabuni.

Sehemu ya Tano inahusu Kanuni za Manunuzi na Uuzaji inajumuisha kutumika kwa kanuni za manunuzi na uuzaji, mipango ya ununuzi na uuzaji, mfumo unaokubalika, mfumo wa uhifadhi, utaratibu mzuri na viwango vinavyokubalika, viwango vya nyaraka za zabuni, uteuzi wa wazabuni, njia za kuwasalisha zabuni, kupokelewa na kufunguliwa zabuni, sifa za msingi za wazabuni, uchanganuzi, kurejeshwa kwa wazabuni, kuzuiliwa kwa baadhi ya maafisa na mambo mengineyo.

Sehemu ya Sita inaeleza Utaratibu wa Manunuzi na Uuzaji ambapo inajumuisha utaratibu wa kuchagua zabuni, zabuni za ndani, zabuni za kimataifa, zabuni za ndani za pekee, zabuni za kimataifa za pekee, utaratibu wa kutoa dondoo za zabuni, ununuzi wa moja kwa moja, ununuzi wa dhamani ndogo, utaratibu wa uuzaji mali za umma, ununuzi wa huduma za ushauri elekezi na mambo mengineyo.

Sehemu ya Saba inaelezea aina za mikataba inajumuisha uchaguzi wa mikataba na aina za mikataba au utaratibu wa kukubaliana.

Sehemu ya Nane inahusu Mapitio ya kiutawala ambayo inajumuisha mapitio ya kiutawala, mapitio na Afisa Masuuli na mapitio ya Mamlaka.

Sehemu ya Tisa inazungumzia mambo ya jumla ambapo inajumuisha ukomo wa mikataba na wahusika wa taasisi za ununuzi na uuzaji mali, kinga ya kutoshitakiwa, kanuni za maadili, makosa na adhabu, kanuni, miongozo na kufuta na kubakiza.

Mwisho kuna Majadweli Manne-

Jadweli la Kwanza linahusu Kiapo cha Tamko;

Jadweli la Pili linahusu Muundo wa Bodi ya Zabuni;

Jadweli la Tatu linahusu Masharti ya Kutumia Njia za Ununuzi; na

Jadweli la Nne linahusu Kanuni za Maadili ya Utendajikazi.

ZANZIBAR
29 Agost, 2016

(DR. KHALID S. MOHAMED)
Waziri wa Fedha na Uchumi
Zanzibar